# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 30 Oktoba, 2007**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma* Dua

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu tarehe 24 Oktoba, 2007 tulimpoteza mwenzetu Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, katika ajali iliyotokea kule Kibena Njombe. Kama ilivyo desturi yetu kabla hatujaendelea na shughuli yoyote nawaombeni tusimame na tukae kimya kwa dakika moja kwa kumbukumbu yake.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumwombea Marehemu Salome Joseph Mbatia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsateni sana. Tunamwomba Mwenyezi Mungu kwa rehema yake iliyo kuu aiweke roho ya mwenzetu Marehemu Salome Joseph Mbatia, mahali pema peponi. *Amen.*

## TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, natoa taarifa kuwa katika Mkutano wetu wa Saba, Bunge pamoja na shughuli nyingine ilipitisha Miswada kadhaa. Katika Mkutano wetu wa Nane, niliwatangazia Miswada iliyokuwa imepata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria. Aidha, wakati huo huo niliwajulisha Waheshimiwa Wabunge, Miswada iliyokuwa haijapata kibali cha Mheshimiwa Rais kutokana na kutokamilika. Nafurahi kusema sasa Miswada hiyo baada ya kukamilika ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais na kupata kibali chake mnamo tarehe 28 Agosti, 2007 na sasa ni sheria. Miswada hiyo ni ifuatayo:-

(i) *The Urban Planning Act, 2007 (No.8/2007);* na

*(ii) The Roads Act, 2007 (No.13/2007).*

Aidha, katika Mkutano wa Nane, Bunge pamoja na mambo mengine lilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali Mitatu. Miswada hiyo baada ya kukamilika nayo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili ipate Kibali chake. Nafurahi kuwaarifu kwamba Miswada hiyo ilipata kibali chake, tarehe 10 Septemba, 2007 na sasa ni Sheria kama ifuatavyo:-

*(i) The Appropriation Act, 2007 (No. 15/2007);*
*(ii) The Finance Act, 2007 (No.16/2007); na*
*(iii) The Higher Education Student's Loans Board (Amend) Act, 2007 (No.17/2007).*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kabla ya kuwasilisha mezani Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali. Naomba kutumia fursa hii kutoa pole na salaam za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wote wa marehemu Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Naibu Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa hakika ajali aliyoipata na hatimaye kifo chake kimetuhuzunisha wengi na kimetuachia majonzi makubwa. "Bwana alitoa na Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe."

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo sasa naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwasilisha mezani.

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

**Mfumo wa Utekelezaji wa Shughuli Kikanda**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. STEPHEN J. GALINOMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimejiwekea mfumo wa utekelezaji wa shughuli zake Kikanda hasa kwa ile Mikoa isiyokuwa na

kanda; na kwa kuwa, mfumo huo husababisha usumbufu na gharama za ziada kwa ile Mikoa isiyo na Makao Makuu ya Kanda kama vile Iringa ambapo hulazimu huduma za Wizara hizo zifuatwe huko yaliko Mako Makuu na wakati mwingine huwa vigumu kupatikana kwa sababu moja au nyingine, ikiwa ni pamoja na ukata wa bajeti za Wizara hizo; na kwa Mkoa wa Iringa, huduma hufuatwa Mbeya:-

(a) Je, Serikali haioni usumbufu unaotokana na gharama za ziada kwa Mikoa isiyo na Makao Mkuu, na ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kila Mkoa unapatiwa huduma hizo bila kutegemea Ofisi za Kanda?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, mfumo huo siyo tu unakuza urasimu, bali unapingana na dhana ya kasi mpya ya kuleta maendeleo na unapingana na dhana nzima ya kusogeza huduma karibu na wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nami kutokana na ukweli kwamba katika miaka mitano ya Chuo Kikuu katika fani ya Udaktari nilikuwa *room mate* wa Dr. Joseph Mbatia na nilitokea kumfahamu Mheshimiwa Marehemu Salome Mbatia akiwa mchumba wake. Naomba niungane kwa niaba ya watu wa Mbozi na Jumuiya ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote katika kutoa pole kwa msiba uliotokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitoe majibu ya swali la Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuunda Kanda za utekelezaji unalenga kuboresha huduma ili zipatikane kwa urahisi na kwa ufanisi na hivyo, kuwezesha kupunguza gharama mbalimbali kwa wananchi. Mara nyingi huduma za kitaalam zinazotolewa huambatana na matumizi makubwa kutoka Makao Makuu, kutokana na upungufu wa wataalam na rasilimali nyingine.

Ni kwa misingi hiyo ndiyo maana baadhi ya Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi za Umma zimeamua kutoa huduma Kikanda. Kwa mfano, Kanda ya Utafiti wa Kilimo iliyopo pale Mbeya, inahudumia Sekta ya Kilimo na Umwagiliaji kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma.

Kuwepo kwa Kanda hiyo, kunasaidia kupata timu ya wataalam wa fani husika kwa karibu zaidi na kuweza kusimamia sekta kufanya kazi kikamilifu. Aidha, mfumo wa Kikanda unaotumiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI umeonyesha mafanikio makubwa katika Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa. Mpango huu unasimamiwa Kikanda na kwa eneo la Nyanda za Juu Kusini Makao yake Makuu yako Mbeya.

(b) Mheshimiwa Spika, mfumo wa Kikanda unaotekelezwa hapa nchini haukuzi urasimu katika mazingira tuliyonayo ambapo raslimali zetu ni chache. Ni vyema tukakubali kwamba jitihada za Serikali kuunda Kanda hizo ni hatua mojawapo ya kusogeza huduma karibu ili zipatikane kwa gharama nafuu na ndiyo inachangia kuwapelekea wananchi maendeleo kwa kasi zaidi.

Azma ya Serikali ya kujenga uwezo wa rasilimali watu na fedha, nyenzo na kuziimarisha Halmashauri zote nchini inalenga kutosheleza mahitaji hayo muhimu kwa Halmashauri, Wilaya na Mikoa na hatimaye kuachana kabisa na mfumo wa Kikanda.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matarajio ya Mikoa yetu yote ni kupata fedha za maendeleo mapema baada ya Bunge kupitisha Bajeti; na kwa kuwa fedha hizo zinapelekwa aidha kidogo au zinachelewa kupelekwa katika Mikoa yetu hasa fedha za barabara na mvua zimekaribia. Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu kupeleka fedha za maendeleo katika Mikoa yetu kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, ni kweli dhamira ya Serikali ni kupeleka fedha za maendeleo katika kila Mkoa kwa wakati na hilo ndilo lengo katika azma yetu ya kupeleka maendeleo yetu kwa haraka. Hivyo basi, Serikali inaahidi kwamba kwa kila namna itajitahidi fedha hizo zifike haraka iwezekanavyo.

Na. 2

**Uhitaji wa Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Kibakwe.**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu wote kutoa salaam za rambirambi kwa msiba uliotupata.

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kibakwe kinapokea rufaa za wagonjwa wengi kutoka katika vijiji 27; na kwa kuwa Kituo hicho kinafanya kazi chini ya kiwango kinachotarajiwa kwa kukosa nyenzo muhimu kama vile majengo ya kutosha, chumba cha kufanyia upasuaji, na kwa kuwa hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa iko mbali sana, na wagonjwa wengi hupoteza maisha hasa akina mama wajawazito na watoto wao wanaposhindwa kujifungua Kituoni hapo kwa kukosa uwezo wa kukodisha magari ya kuwapeleka hospitali ya Wilaya, na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa haina uwezo wa kutosha wa kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo hicho:-

Je, Serikali itatoa msaada gani wa dharura ili kupata gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Kibakwe ili kunusuru maisha ya wagonjwa yanayopotea kutokana na kukosekana kwa huduma hiyo ya usafiri wa kuwawahisha kwenye hospitali ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kibakwe kinatoa huduma za afya kwa watu wapatao 71,405. Kulingana na mwongozo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kituo cha Afya chochote kinapaswa kutoa huduma kwa watu wapatao 50,000 hadi 100,000. Kwa mantiki hiyo idadi ya watu wanaopata huduma katika Kituo cha Afya cha Kibakwe ni wastani wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya kinapaswa kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje *(OPD)*, wagonjwa wanaolazwa *(IPD)*, huduma kwa wajawazito na upasuaji mdogo na pia kutoa huduma za maabara zikiwemo kuongeza damu kwa wagonjwa wenye kuhitaji kuongezewa damu.

Ili kuweza kutoa huduma hizo Kituo cha Afya ni lazima kiweze kuwa na jengo la wagonjwa wa nje kwa ajili ya huduma za kawaida, wodi mbili kwa ajili ya wanawake na wanaume, wodi ya wajawazito, wodi ya watoto, chumba cha upasuaji, chumba cha maabara pia iwepo sehemu ya ufuaji na chumba cha kuhifadhi maiti. Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuhakikisha kuwa wananchi wake wakiwemo wakazi wa Kibakwe wanapata huduma zilizo bora na kwa wakati muafaka. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imeanza kuchukua hatua za kuboresha huduma za Kituo cha Afya cha Kibakwe kwa kufanya ukarabati wa chumba cha upasuaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006 ilinunua magari 30 ya kubeba wagonjwa, na kwa mwaka 2006/2007 ilinunua magari 33 ya kubeba wagonjwa. Wilaya ya Mpwapwa ni mojawapo ya Wilaya zilizopewa gari la kubeba wagonjwa *Toyota Land Cruiser* lenye namba za usajili SM 5082. Gari hili limekuwa likitoa huduma za dharura kwa Vituo vya Afya ndani ya Wilaya hiyo kikiwemo Kituo cha Afya Kibakwe. Pia gari lenye namba za Usajili SM 2992 *Toyota Land Cruiser* ambalo liko Kituo cha Afya cha Rudi kilichoko umbali wa Kilomita 45 kutoka Mpwapwa limekuwa likitumika kutoa huduma za usafiri kwa Kituo cha Afya Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imeidhinisha fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari la kubeba wagonjwa kwa ajili ya hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa. Ununuzi wa gari hili utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la usafiri kwa Kituo cha Afya Kibakwe. Serikali itaendelea kununua magari ya kubeba wagonjwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha katika Halmashauri

ambazo hazijapata badala ya kuziongezea Halmashauri ambazo zimekwishapata kama vile Mpwapwa. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuweka utaratibu katika bajeti zao fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, katika swali la msingi nilizungumzia ombi la gari kama mbadala tu kwa huduma nzuri katika Kituo cha Afya cha Kibakwe. Lakini jambo la msingi hapa ni namna gani Serikali ipo tayari kutusaidia kukipanua kile Kituo cha Afya cha Kibakwe kiweze kutoa huduma kama alivyotaja; kwa kuwa, kwa sasa kinatoa huduma chini ya kiwango hicho, na kwa uwezo wa Halmashauri Bajeti tuliyoipanga ni fedha kidogo sana ambayo haiwezi kutusaidia. Je, Serikali ina mpango gani kutusaidia kupata fedha nyingine?

La pili, ni kuhusiana na gari ambalo tumepewa. Gari tuliyopewa litakuwa likikaa pale Wilayani Mpwapwa. Juzi juzi mimi mwenyewe nilikuwepo pale Kibakwe mama mjamzito akafariki na nikiwa ninajitahidi kumsaidia kumpeleka Mpwapwa. Kwa hiyo, gari likiwa Mpwapwa linaweza pia lisitusaidie? Naibu Waziri yupo tayari kutusaidia kutupa gari ambayo itakuwepo pale pale Kituo cha Afya cha Kibakwe kwa sababu ni vijiji vingi vinaizunguka Kibakwe na Mpwapwa ni mbali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kupata fedha za ziada kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya cha Kibakwe, kama nilivyosema ni kwamba Kituo cha Afya hicho tumeanza kukipa fedha kwa awamu ili kukikarabati na kukiongezea uwezo zaidi. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwamba Serikali ina nia nzuri tu ya kupanua huduma za afya kwa Vituo vya Afya vilivyopo na vile ambavyo vinaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inagawa magari kwa kila Wilaya na Wilaya ikishapata hilo gari ni hiari yao aidha kuliweka katikati ya Hospitali ya Wilaya au kuipeleka kwenye Kituo cha Afya kimoja. Sisi tuliona kama gari ni moja na Vituo vya Afya vipo vitano, ni vyema lile gari likakaa Makao Makuu yaani kwenye Hospitali ya Wilaya ili wale wanaohitaji katika Vituo vya Afya mbalimbali waweze kupatiwa huduma. Tulichofanya ni kuwaambia wenzetu wa Halmashauri kuhakikisha kwamba kila Kituo cha Afya kina *Radio Call* ili wakihitaji hilo gari waweze kuwasiliana na Wilaya, gari liende likawachukue wagonjwa na lirudi tena katika hospitali ya Wilaya.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Pamoja na pongezi kwa Serikali kwa sera hii nzuri ya kupeleka magari ya wagonjwa katika Wilaya mbalimbali hapa nchini ambapo baadhi ya magari hayo yamekuwa katika Vituo vya Afya vilivyo mbali na Wilaya. Swali langu linahusu agizo la Serikali ambalo lilisikika hivi karibuni kwamba magari hayo ya wagonjwa ni marufuku kwa wananchi kuchangia mafuta katika vyombo vya habari.

Nia ya swali langu ni kupata ufafanuzi endapo jambo hili lipo sawasawa kwa kesi kama hii ya Kibakwe ambapo unaweza ukawa na gari lakini mafuta hakuna kwa wakati huo, hali itakuwa namna gani. Je, Serikali imepeleka Bajeti ya kutosha kuhakikisha kwamba magari hayo yana mafuta masaa yote na wakati wote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kwamba magari yote haya yawe na mafuta kwa wakati wowote. Lakini Bajeti wakati mwingine hairuhusu. Kwa hiyo, wakati mwingine inabidi wananchi wenyewe wajitolee, lakini kinachotakiwa baadaye warudishiwe zile fedha. Kwa hiyo, ufafanuzi ule ni wa ukweli alioutoa Mheshimiwa Waziri kwenye vyombo vya habari kwamba kila Halmashauri ijitahidi kwa kadri ya uwezo wake kuhakikisha kwamba magari hayo yanakuwa na mafuta wakati wote.

**SPIKA:** Uhandisi, leo *mic* nyingi sasa hazifanyi kazi. Upande huu imetokea na huku tena.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Swali langu lilikuwa linafanana sana na la Mheshimiwa Job Ndugai, hasa kwa kuangalia kwamba eneo la Liwale ni *square* kilomita 39,000 na siyo hivyo tu, vyanzo vyake vya mapato ni kidogo mno.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge naomba ukae chini kwa sababu hamwezi kusimama wawili, swali linaulizwa na mtu mmoja. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Chanzo cha mapato cha Wilaya ya Liwale ni kidogo mno. Sasa kama kweli Serikali inadhamiria kufanya hivyo ilivyotangaza na mimi nilikuwa ni mmojawapo wa kufuatilia kwa karibu kuona tunafanya nini kwa Wilaya ya Liwale, vinginevyo ingeweza kutuletea vurumai na wananchi kwa suala ambalo halitekelezeki. Ningeomba Serikali itusaidie watu wa Liwale na wa maeneo hayo mengine ambapo maeneo yao ni makubwa na kipato cha Halmashauri ni kidogo tofauti na kama ilivyo Wilaya ya Temeke, ukituma gari katika Wilaya hiyo haina tatizo. Lakini Wilaya ya Liwale ina *square* kilomita 39,000 jamani ni nyingi na uwezo huo haupo. Naomba kupata maelezo zaidi ya ziada.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya ziada ya ufafanuzi kuhusiana na suala hili la magari ambapo Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo wameliulizia.

Mheshimiwa Spika, magari ya wagonjwa haya ni magari ya Serikali kama yalivyo magari mengine katika kila Halmashauri yanatakiwa yahudumiwe na Halmashauri kwa maana ya matengenezo ya gari linapokuwa ni mbovu, linapaswa kupewa mafuta kama magari mengine yanavyopewa mafuta kwa kazi nyingine katika

Halmashauri.  Ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha magari hayo yanatoa huduma hiyo kulingana na maelekezo  ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lazima tukumbuke vile vile unapokuwa ni mgonjwa halafu unategemewa tena utafute fedha ili uweze kwenda hospitali kwa kweli  lengo la Serikali la kutoa huduma hii kwa ajili ya Watanzania wagonjwa halitakuwa limekamilika. Kila Halmashauri ijipange vizuri  na mimi ninaamini inawezekana kabisa kwa sababu sehemu zote waliojaribu wamefanikiwa.

**SPIKA:** Ninaona ni haki nitoe nafasi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, si ajabu yeye ndiye aliyetoa tangazo hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, sijatoa. Ninaomba kuongezea majibu mazuri yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, sasa hivi inaandaa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, na katika Mpango huo ambao tutaufanya ni kwamba kila Kituo cha Afya kutakuwepo na *theatre* ndogo ambapo hiyo itakuwa inashughulikia *emergence of optheatic  care*. Kwa maana  hiyo katika vile Vituo vya Afya ambavyo tunaona vipo mbali tutajenga *theatre* ndogo ambapo pale operesheni na hasa  za  akinamama ambao wana matatizo ya uzazi wataweza kushughulikiwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo Mpango huu wa Maendeleo ya Afya ya Msingi tutauanza  mwaka 2008/2009 na ni Mpango ambao utachukua miaka 10.

Kwa hiyo, naamini kabisa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itajipanga ili kuweza kuangalia kwamba  yale maeneo ambayo ni magumu zaidi tutawapatia hizo *theatre* ili operesheni hizo zifanyike pale na wale watakaoshindakana zaidi watapata rufaa  sasa za kwenda katika hospitali za Wilaya ambapo watapata huduma zaidi. Nashukuru.  *(Makofi)*

Na. 3

**Matetemeko ya Ardhi**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza**:-**

Kwa kuwa katika kipindi cha miaka ya karibuni, maeneo kadhaa hapa nchini yamekuwa yakikumbwa na matetemeko ya ardhi kama Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na Rungwe Mkoani Mbeya, hali iliyojenga hofu kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kutambua dalili za kutokea kwa maafa kama hayo?

(b) Je, Serikali inatoa tahadhari gani kwa kwa wananchi waishio katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (*Geological Survey of Tanzania*) imeweka vituo vinane vya kudumu na vituo vitatu vya muda kwa ajili ya kupima matetemeko ya ardhi katika maeneo ambayo mara kwa mara huathirika. Vituo vya kudumu vipo Mahale katika Mkoa wa Kigoma, Panda Hill Mkoani Mbeya, Singida Mjini na Manyoni Mjini Mkoani Singida, Kondoa Mjini na Dodoma Mjini Mkoani Dodoma, Kibaya katika Mkoa wa Manyara na Longido Mkoani Arusha. Vituo vya muda vimewekwa kuzunguka Ziwa Natron na viko Engaruka, Ngaresero na Kitumbaine, mahususi kupima eneo hilo ambalo limekaribiwa na matetemeko ya ardhi tangu mwezi Juni, 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa taarifa za matukio hayo na kuwatahadharisha wananchi wa maeneo husika kupitia vyombo vya habari mbalimbali. Mfano, wakati wa matetemeko yaliyotokea kuzunguka Ziwa Natron Mkoani Arusha, tarehe 20 Julai, 2007 wakati wa Mkutano wa Nane, Kikao cha Ishirini na Nane, Waziri wa Nishati na Madini alitoa Kauli za Mawaziri kuhusu matetemeko ya ardhi yaliyoyakumbua maeneo ya Kaskazini mwa nchi yetu na kuwatahadharisha wananchi jinsi ya kuepukana na madhara yanayosababishwa na matetemeko ya ardhi. Aidha, Waziri aliwataka wananchi wanaoishi kuzunguka Mlima Oldonyo Lengai wahame na kwenda kwenye maeneo yaliyo umbali wa zaidi ya kilomita 50 kutoka mlima huo.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Serikali hutembelea wananchi wa maeneo yaliyokumbwa na matetemeko na kuwashauri hatua za kuchukua. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea eneo la Mlima Oldonyo Lengai tarehe 23 Agosti, 2007 na kutoa maelekezo na tahadhari kwa wananchi wa eneo hilo. Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Maafa) Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na Naibu Waziri Nishati na Madini walitembelea eneo hilo la Mlima Oldonyo Lengai, tarehe 23 hadi 25 Julai, 2007 na kuongea na kutoa ushauri kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunatoa rai na kuwatadharisha baadhi ya wananchi ambao wamekuwa wakiharibu au kuiba vifaa vya kupima matetemeko kama ilivyotokea Songea, Tabora, Ntyuka Dodoma na Longido Arusha waache tabia hiyo. Aidha, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kushirikiana na Serikali kulinda na kutunza vifaa hivi.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninashukuru sana kwa majibu fasaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na hivyo, naomba kumwuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mara nyingi matetemeko yakitokea yanaleta maafa makubwa, na hasa kwa kubomolewa nyumba za wakazi wa maeneo hayo. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuwaangiza wataalam waweze kubuni au kutoa michoro maalum ya nyumba zinazofaa kujengwa katika maeneo hayo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati wa kuwa na Mfuko maalum kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanaopata matatizo yanatokana na matatemeko hayo ili waweze kupata misaada ya haraka wakati maafa hayo yanapotokea?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la nyongeza kuhusu michoro ushauri ni mzuri nikiri tu kwa niaba ya Serikali kwamba tumeupokea tutaendelea kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika hili suala la michoro ama nyumba zipi zijengwe katika maeneo ambayo mara kwa mara yamekuwa yakiathirika linahitaji utafiti na uchunguzi wa kina kwa sababu matukio haya hayatoi viashiria vya awali kwa kipindi ambacho kinaiwezesha Serikali kuweza hasa kubuni kwa sababu ni matukio ambayo yanatokea bila ya kutarajiwa. Lakini kama nilivyosema ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tunaupokea.

Kuhusu sehemu ya pili ya swali kwamba Serikali haioni kuwa na Mfuko maalum naomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kuliarifu Bunge hili Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali siku zote ina mipango maalum na kwa kweli katika hili suala la maafa tayari ina kitengo ambacho kinashughulikia maafa na ikijitokeza kwamba kuna waathirika katika maeneo ambayo yamekumbwa na matetemeko ya ardhi ni jukumu la Serikali kwa kweli kuchukua hatua tu kama ambavyo imekuwa ikijitokeza na inaendelea kufanya hivyo kwa sababu maafa ni maafa kuna kitengo maalum watendaji wakuu wa Serikali wapo na tutaendelea kulishughulikia kadri ambavyo linajitokeza. Kwa hivi tunaihakikisha Bunge Tukufu na wananchi kwamba Serikali imejipanga na imekuwa ikifanya hivyo na utaratibu upo wa kuwasaidia waathirika. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matetemeko ya ardhi yanatokea pia baharini kama hivi karibuni yalivyotokea katika nchi za Asia. Na kwa kuwa makazi mengi ya watu katika ukanda wa bahari kuanzia Mtwara mpaka Tanga na Visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia. Je, *geological survey* ya Tanzania imeweka vituo gani vya kuonesha dalili ya matetemeko huko ambapo kuna kazi kubwa na mahoteli mengi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba sasa hivi *geological survey of Tanzania* haijaweka vituo baharini. Lakini kwa sasa hivi kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifaa *geological survey of Tanzania* ina mahusiano hususan na Taasisi za Kimarekani na hata matetemeko ambayo yanapimwa hapa Tanzania tunatumia utaalamu wa Taasisi za Kimarekani na baada ya kutokea haya matetemeko makubwa ambayo yameikumba baharini kuna vituo vingi ambavyo vimewekwa baharini na tutaendelea kuwa na ushirikiano na Taasisi hizo za Kimataifa kusudi panapotokea matetemeko hayo waweze kututolea maangalizo ya awali kama ilivyotokea juzi juzi tulikuwa tumeshapata taarifa na kutoa maangalizo hapa Tanzania kwenye watu wanaokaa kwenye ukanda wa baharini wakaweza kusogea sehemu salama.

Na. 4

**Hitaji la Kivuko cha Kisasa – *Rusumo Border***

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kivuko cha *Rusumo Border* kinahatarisha maisha ya wafanya kazi wa Kata za Nyamiyaga na Rusumo kwa kusababisha maafa mara nyingi kwa wafanyakazi wa Kivuko hicho waliotumbukia mtoni na kufa:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka kwa kununua Kivuko cha kisasa kinachoendeshwa kwa umeme badala ya kilichopo kilichoachwa na mkoloni, ambacho ni cha zamani kinachovutwa na kamba kwa kutumia nguvu za watu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feetham Fillipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Kivuko cha Rusumo chenye ukubwa wa tani 7 kina uwezo wa kubeba gari moja na abiria 50 kwa wakati mmoja. Kivuko hiki kilitengenezwa wakati wa mkoloni na kinafanya kazi kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni. Kivuko hiki kinamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na kinaunganisha mji wa Rusumo na sehemu zingine za Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Feetham Fillipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Kwa sasa Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kuchukua kivuko hicho kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Aidha, Wizara itatenga fedha kwa ajili ya kununua kivuko kipya kinachojiendesha chenyewe katika Bajeti yake ya mwaka 2008/2009.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Matatizo yaliyoko Rusumo yanafanana sana na matatizo yaliyoko Busisi katika kivuko kinachokwenda Geita. Kivuko cha Busisi kimekuwa kama ndoto tumekuwa tukiahidiwa kwenye Mkutano wa Barabara wa Mkoa tukaambiwa mwezi Januari, baadaye tena tukaambiwa mwezi Mei, Rais naye akaenda akaambiwa mwezi Julai kitakuwa tayari. Sasa napenda niambiwe ni lini kivuko hicho kitakuwa tayari kwa sababu mauaji yameshatokea karibu mara mbili kwa sababu ya kukosa kivuko hicho? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na sababu za kiufundi na matatizo mengine yaliyojitokeza kwa upande wa Mkandarasi anayejenga kile kivuko zile ahadi za kivuko kukamilika mapema hazikuweza kutimizwa. Lakini kwa taarifa ambazo sasa tunazo Mkandarasi atakamilisha kazi zote na kivuko kujaribiwa ndani ya miezi kama miwili hivi ijayo nadhani tutakuwa tumekamilisha. *(Makofi)*

Na. 5

**Ubora wa Elimu – Shule za Kata**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetoa kipaumbele katika elimu kwa kuhakikisha kuwa kila Kata ina Shule mpya ya Sekondari na kwa kuwa wanafunzi walioanza Kidato cha Kwanza mwaka 2006 watafanya Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2010; na kwa kuwa mtihani watakaofanya unafanana kwa shule zote (zile za Kata na za zamani zilizo na nyenzo za kutosha):-

(a) Je, Serikali itahakikishaje kuwa inatenda haki katika mitihani hiyo kwa wanafunzi wa Sekondari mpya za Kata, ambao hawana nyenzo za kutosha ikilinganishwa na wenzao wa shule za zamani au za binafsi zilizo na nyenzo zinazotakiwa hapa nchini?
(b) Pamoja na nia njema ya kupeleka watoto wengi Sekondari. Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata elimu iliyo bora ya kuwawezesha kumudu ushindani wa kielimu katika dunia hii ya utandawazi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya Shule za Sekondari hazina nyenzo za kutosha za kuwezesha shule kuwa na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali imeweka vipaumbele katika:-

Ujenzi wa nyumba za walimu. Shilingi Bilioni 13.5 zimetengwa kuchangia ujenzi wa nyumba 1,500 ili kuwawezesha walimu wakae kwenye maeneo yao mazuri.

Kutoa Ruzuku ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia shilingi Bilioni 9.14 zimetolewa.

Kutoa mafunzo kazini ili kuimarisha walimu katika ufundishaji. Zimetengwa sh. Bilioni 11.1 zimetolewa.

Kutoa ruzuku ya fidia ya ada ambayo pia hutumika kununulia vifaa vya shule shilingi Bilioni 10 zimetolewa.

Katika mwaka 2008 Serikali ina mpango wa kuongeza idadi ya Maabara kwa kusaidiana na *ADB.* Aidha, tunafuatilia upatikanaji wa vivunge vya sayansi (*science kits*) kama njia ya kusaidia kufanya mazoezi kwa vitendo tukisubiri Maabara kujengwa. Tunawashukuru viongozi na wananchi kwa kuhamasika katika ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata, tunaomba tuendelee kushirikiana ili kuhakikisha kuwa shule hizo zinakuwa na mazingira bora katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa kwa Watanzania, mambo muhimu yanayohitajika ni pamoja na; walimu wenye sifa za kutosha, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na Maabara. Aidha, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata elimu bora kama ifuatavyo:-

Kuongeza idadi ya walimu kwa kuongeza nafasi zaidi katika Vyuo vya Ualimu ngazi ya Stashahada.

Kubadilisha Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na Shule ya Sekondari ya Mkwawa, kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Elimu ambavyo pamoja na Vyuo Vikuu vingine vinavyoanzishwa nchini vitatoa walimu wengi watakaokidhi mahitaji ya walimu katika Shule za Sekondari mwaka 2008. Katika mwaka 2008 walimu takribani 12,000 wa Stashahada na Shahada wanatarajiwa kuhitimu.

Kama ilivyotajwa katika (a) kuimarisha mafunzo ya walimu kazini *(In-Service Training)*, ikiwa ni pamoja na kuwaendeleza walimu wa leseni.

Kutoa ruzuku ya Maendeleo ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na fidia ya punguzo la ada.

Kutoa ruzuku ya ujenzi wa nyumba za walimu, vyumba vya madarasa, Maabara na Hosteli.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona mmesahau kwamba lazima kadi kwanza.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mojawapo ya mahitaji ya elimu bora ni pamoja na vitabu. Sasa nauliza, je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha vitabu vipo hata kama ni vya kununua lakini vipo katika maeneo ya shule kwa wingi kama vile wanafunzi ambapo sasa hivi wanakwenda katika Shule za Sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kuna suala la Wizara kutoa fedha za ruzuku ya maendeleo ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na fidia ya punguzo la ada. Hizi fedha zinapofikishwa shuleni Bodi ya Shule pamoja na Mwalimu Mkuu pamoja na walimu wanakaa wanapanga kununua vitabu vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi katika shule yao. Wizara imepeleka jukumu hili katika kila shule ili waweze kununua vifaa. Hivyo si kazi tena ya Wizara kununua vifaa na kuvisambaza mashuleni kwa sababu ya uwingi wa shule tunazokuwa nazo na tuliona huu ndio mpango mzuri ambao tukipeleka fedha itakuwa rahisi kwao kama shule wao kujipangia kununua vile vitabu wanavyovihitaji kwa ajili ya kufundishia pale shuleni.

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa moja kati ya mambo ya msingi katika suala zima la kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu ni pamoja na umbali mdogo anaopaswa kutembea mwanafunzi kutoka anakotoka kwenda shuleni. Na kwa kuwa kwa jiografia kama ya Wilaya ya Simanjiro ambayo ni kilomita za mraba 20,000 na umbali kati ya kijiji hadi kijiji ni kati ya kilomita 40 mpaka 70. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba shule hizi za Kata zinazojengwa katika Wilaya zinazofanana na Simanjiro zinatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli au mabweni ili kuboresha mazingira ya watoto hao kupata elimu na kuweza kushindana na wengine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, hili suala la wanafunzi kutembea mwendo mrefu linajulikana wazi na ndiyo maana wananchi na wazazi wamekuwa wakihimizwa katika Shule za Sekondari za Kata waendelee kujenga hosteli hasa kwa ajili ya Wasichana ambao wanaishi katika mazingira magumu hasa kwa kupanga katika nyumba za wananchi vijijini. Tunashauri wananchi na wazazi waendelee kujitolea kujenga hosteli ili waweze kukaa katika mazingira karibu na shule. Lakini Wizara yangu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeweza kutoa fedha kwa ajili ya kujenga hosteli katika maeneo ya wafugaji katika shule tano. Huu ni mwanzo tutaendelea kuangalia mahitaji ya maeneo na jinsi ambavyo wananchi wenyewe wanajitolea kutaka kusaidia katika ujenzi wa hosteli katika mazingira kama hayo. *(Makofi)*

Na. 6

**Wanafunzi Wanaobeba Mimba Shuleni**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, pamoja na adhabu ya kuwafukuza shuleni wasichana wanaopata mimba, kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaobeba mimba mwaka hadi mwaka:-

(a) Kwa kulinda haki ya msingi ya kupata elimu. Je, Serikali itakubali iwepo sheria itakayowaruhusu wanafunzi wanaobeba mimba kurejea mashuleni mara baada ya kujifungua kama baadhi ya nchi nyingine zinavyofanya?

(b) Kwa kuondoa sura ya ubaguzi katika kutoa adhabu na pengine kupunguza ongezeko la wanaobeba mimba. Je, Serikali haioni muhimu wa kusambaza mashine za *DNA* ili kuwatambua wanaume wanaowapa wanafunzi mimba ili nao waadhibiwe?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Elimu ni Haki ya Msingi kwa wote wakiwemo wasichana. Serikali kupitia Wizara yangu kwa kuzingatia uzito wa jambo hili katika mwaka huu wa fedha, imeibua mjadala wa Kitaifa kuhusu tatizo la mimba kwa wanafunzi wenye lengo la kupata maoni kuhusu jinsi ya kuzuia, kuwashughulikia wanaohusika na pia kuangalia uwezekano wa kuwarejesha shuleni baada ya kujifungua. Endapo kupitia mjadala huo, jamii ikiridhia suala hilo, Serikali itachukua hatua zinazostahili za utekelezaji wake kama zilivyoruhusu nchi nyingine zikiwemo Zambia na Malawi. Lakini ni vyema jamii ikaelewa umuhimu wa kuzingatia maadili mema kwa wanafunzi ili kuepukana na utovu wa nidhamu na hatari za maambukizi ya UKIMWI nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, ipo sheria ya adhabu kwa wanaowapa mimba wanafunzi. Aidha, katika mjadala ulioibuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mambo yanayojadiliwa ni pamoja na kuangalia namna ya kukazia sheria ya kuwaadhibu wanaowapa mimba wanafunzi. Kutumika kwa mashine za *DNA* za kuwatambua wanaume wanaowapa mimba wanafunzi na kisha kukataa kutasaidia sana. Kwa hiyo, tutawaomba wenzetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii waweze kusambaza mashine hizo, ili wanaobainika nao waadhibiwe.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niulize swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo hili la kutoa mimba watoto linaongezeka siku hadi siku, pamoja na sheria iliyopo lakini bado inaonekana vijana wanashika kasi. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kutoa adhabu kali ya kuwanyonga hawa hadharani ili iwe ni fundisho? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge kutolewa adhabu kali ya kuwanyonga wale wanaowatia mimba wasichana wanaosoma shule tena wanyongwe hadharani Serikali hatujafikia hapo.

Hili ni tatizo la kijamii lakini tunajua kabisa kwamba kuwakosesha wasichana masomo ni kosa kubwa kwa sababu hawa watu wangeweza wakimaliza masomo wawe wananchi bora katika nchi yetu.

Lakini tatizo hili kwa sababu ni la kijamii ni suala la wananchi kila mmoja wetu awajibike ipasavyo kuwalinda hawa wasichana lakini na wasichana wanao wajibu wa kufahamu kwamba kutenda jambo hili kisiri ni kosa kwa sababu jamii inakataza na wazazi huwa hawapendelei kitendo cha namna hii kikitokea na ndiyo maana tumeanzisha mjadala ili wananchi washiriki katika mjadala huo tuweze kuona ni hatua gani bora zichukuliwe na ikiwezekana pia tujadili tuone ni adhabu gani itakayofaa kutolewa lakini hii ya kunyongwa hadharani hapana, sidhani kama Serikali itakubaliana nayo. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Martha M. Mlatta!!!!!? Huyu mwenzetu kwa kuwa alikuwa mbali Uingereza muda mrefu naona amesahau kabisa. Kwa hiyo, nimemwona Mheshimiwa Susan Lyimo swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa sababu kubwa ya mimba za watoto wa shule ni pamoja na kutokuwa na elimu ya afya ya uzazi yaani kutokuwa na *Curriculum* ya afya ya uzazi pamoja na *life skills* kwa wanafunzi hao na ndio sababu utaona *drop out* ipo zaidi kwa watoto wa Shule za Msingi kuliko Shule za Sekondari na Vyuo.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba somo la elimu ya afya ya uzazi pamoja na *life skills* linawekwa katika Shule za Msingi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, elimu ya uzazi katika Shule za Msingi inaanza kufundishiwa kuanzia darasa la tatu. Kwa hiyo, ipo inafundishwa cha msingi labda ni kuangalia jinsi gani ya kuimarisha zaidi, lakini inafundishwa katika Shule za Msingi kuanzia darasa la tatu. *(Makofi)*

Na. 7

**Mlipuko wa Volcano – Oldonyo Lengai**

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA (K.n.y. MHE. KAIKA S. TELELE)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa maelezo ya wakazi wa eneo la Oldonyo Lengai (Mlima wa Mungu). Mlima huo hulipuka kila baada ya miaka kumi (10) au kumi na mitano (15); na kwa kuwa mwezi Julai 2007 mlipuko huo uliambatana na tetemeko la ardhi katika eneo zima la Ziwa Natron na Bonde la Ufa, na kwa kuwa hali hiyo ilitangazwa sana na vyombo vya habari vya nje kama *KBC* na *BBC:-*

(a) Je, mlipuko huo wa Volcano ni maafa au kivutio cha utalii?
(b) Je, kutangazwa sana huko kwa tukio hilo na *KBC* ni kwa nia njema au ni katika dhana ya kuwaogopesha watalii wasitembelee Tanzania kwa kuwa wao ni washindani wetu wa kudumu katika biashara ya utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mlima wa Oldonyo Lengai umekuwa ukitangazwa kupitia machapisho ya Wizara pamoja na yale ya Kampuni Binafsi, kama unavyotangazwa Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru na kadhalika. Tofauti na Milima mingine, Mlima Oldonyo Lengai una sifa ya kuwa na *Volcano* Hai (*Active Volcano*) hali ambayo iko kwenye milima michache. Mwaka huu wa 2007 mlima huo ulilipuka na mlipuko kuandamana na tetemeko la ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mlipuko wa *Volcano* ni jambo la hatari lakini unaweza kuwa kivutio cha utalii kufuatana na utashi wa mtu. Utafiti umeonyesha kuwa kuna baadhi ya matukio na majanga ya asili yamekuwa kivutio cha utalii. Mathalan, baada ya tukio la Septemba 11 wageni wanaofika New York wanatembezwa eneo la *World Trade Center* ambapo taswira mbalimbali za yale majengo mawili zinauzwa kwa bei kubwa na watu wananunua kwa wingi.

Hivyo basi, mlipuko wa Oldonyo Lengai unaweza kuwa kivutio cha utalii wanaopenda udadisi, utafiti na wataalam wa mambo ya jiolojia.Kwa kuangalia takwimu za milipuko muda kati ya mlipuko mmoja na mwingine si rahisi kutabirika. Kwa mfano matetemeko na milipuko midogo ilitokea mwaka 1983, 1986, 2005 wakati milipuko mikubwa ilitokea mwaka 1966, 2006, 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, kutangazwa sana kwa tukio hilo na Shirika la Habari la Kenya (*Kenya Broadcasting Corporation – KBC)* hakuwezi kuchukuliwa moja kwa moja kwamba ilikuwa kwa lengo la kuwatishia watalii ili wasitembelee Tanzania. Kwa taarifa, kufuatia matangazo ya vyombo vya habari vikiwemo vya hapa nchini, watalii wengi walitembelea eneo hilo. Aidha, watafiti wa hapa nchini waliongezeka vilevile watafiti wa Marekani na Ujerumani walikuja kutafiti katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara yaliyotokea katika mlipuko wa mwaka huu, yafuatayo yamefanyika.

Mitambo kwa ajili ya kupima matetemeko ijulikanayo kama "*seismo gram*" imefungwa katika maeneo ya Engaruka, Ngaresero, Longido na Ketumbaine.

Wakala wa Jiolojia Tanzania kwa kushirikiana na *Royal Observatory Center* ya Ubelgiji wanapima ongezeko la joto kwa kutumia rada.

Serikali imewashauri wakazi wa maeneo yanayozunguka mlima huo kuhamisha makazi yawe zaidi ya kilomita 50 toka kilele cha mlima huo. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wakazi wa eneo linalozunguka Oldonyo Lengai wameshauriwa kuhama zaidi ya kilomita 50 kutoka pale walipokuwa au kutoka eneo la *Volcano.* Na kwa kuwa kuhama huko kwenda kuanza makazi mapya ni gharama Serikali imeweza kuwasaidiaje wakazi hao waliolazimika kuhama na ambao wamelazimika kuhamia vijiji vya Wilaya ya Ngorongoro, Longido na Monduli.

Mheshimiwa Spika, suala la pili dogo kwa kuwa *Volcano* hii imekuwa ikitokea mfululizo mwaka 2005, 2006, 2007 na kwa kuwa mwaka jana athari hii ilikuwa kubwa kidogo tofauti na huko nyuma na watu wengine waliathirika. Je, Serikali inaweza kutueleza ni watu wangapi ambao waliumia au walipoteza maisha yao kutokana na *Volcano* hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba yale maeneo ambayo watu walibidi kuhama hawakuwa wengi sana, isipokuwa yalikuwa ni maeneo ambayo yalikuwa ya makazi ya wakazi wachache na mifugo ambao wenyewe waliweza kuhama

kwa hiari yao wakahamisha mifugo lakini walikuwa wameacha majumba yao. Kwa sasa hivi maeneo ambayo wamekwenda Serikali ya Mkoa wa Arusha na Wilaya husika hawa watu wamekwenda maeneo salama na wale ambao watakuwa na matatizo wameondolewa matatizo yao.

Swali la pili ambalo linahusu kwamba matetemeko hayo yanatokea mfululizo mara kwa mara bila tahadhari. Kama tulivyokwishasema katika majibu yetu kwamba wananchi wanabidi wachukue tahadhari. Ukubwa wa tetemeko hauwezi ukatabiriwa isipokuwa ni kuhakikisha kama kuna wananchi ambao wako maeneo ambayo wakipata tu taarifa kwamba kutoka Serikalini wazitekeleze mara moja. Kwa mwaka huu tumeona kwamba hata taarifa tuliyoitoa kwamba wananchi wakae kilomita zaidi ya 50. Wananchi wamechukua muda mrefu sana kutekeleza hilo na mpaka tu yale majivu yalipojitokeza kwa wingi na mifugo ilipoathirika ndipo ikabidi wahame.

**SPIKA**: Kabla hatujaendelea kuna Waheshimiwa Wabunge wameniandikia kwamba miswada ya leo itakayozingatiwa leo hawaioni. Ukweli ni kwamba Mswada wa *Public Service Act* umeambatanishwa na Muswada wa *Tourism Act*. Kwa hiyo, usione kitabu hiki ukadhani lote hili ni *Tourism Act.* Kwa kwenye Ukurasa wa 42 wa hiki kitabu ambacho mbele ni *Tourism Act* ndiyo unaanza Mswada wa *Public Service Act*. Natahadharisha sasa ili isifike wakati wa saa nne na nusu mkawa hamjaiona. Ule mwingine wa *Miscellaneous Amendment No. 2 2007* upo ukurasa wa 30 nyuma ya Mswada ambao ni *Environmental Health Practitioners Bill 2007*. Kwa hiyo, yote ipo.

Kwa bahati mbaya inaelekea kuna *Order Papers* zimeandikwa tarehe 30 Agosti, 2007 ni dhahiri hilo ni kosa tu la uchapaji, ambalo limetokea. Leo ni tarehe 30 Octoba, 2007. Tunaendelea na Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Kwa niaba yake Mheshimiwa Anna Lupembe.

Na. 8

**Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia.**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. DR. CHRISANT MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Ili kwenda na karne ya 21 katika Sayansi na Teknolojia Serikali inafanya juhudi gani ya kusomesha wanasayansi ndani na nje ya nchi ili kujiletea maendeleo na kuondoa umaskini hasa tukijifunza kwa watu wa China, India na nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mzindakaya kwamba ili kwenda na karne ya 21 katika Sayansi na Teknolojia ni lazima nchi yetu isomeshe wanasayansi wa kutosha. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu tayari imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Wizara imeamua kuwapatia mkopo wanafunzi wote waliopata udahili katika Vyuo vya ndani katika fani zote za Sayansi na Teknolojia. Aidha Wizara iko katika mkakati wa uanzishwaji wa Taasisi ya Kimataifa ya Sayansi na Teknolojia itakayojulikana kwa jina la "*The Nelson Mandela African Institute for Science and Technology Arusha campus*" kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa wataalam wa Kimataifa katika masuala ya Sayansi na Teknolojia *(S&T)* Utafiti na Maendeleo (*UMA*)

(ii) Mheshimiwa Spika, aidha pamoja na juhudi zinazofanywa na Wizara katika vyuo vilivyopo nchini pia Wizara yangu inapeleka wanafunzi nje ya nchi kwa kutumia *scholarship* za nchi wafadhili na mkazo zaidi huwekwa katika masomo ya sayansi. Mpaka kufikia mwaka huo 2007/2008 Wizara inasomesha nje ya nchi jumla ya wanafunzi 832 katika nchi mbalimbali zikiwemo Afrika Kusini, Algeria, China, *Czech Rep*, Cuba, India, Poland na Urusi. Kati ya hao wanafunzi 654 wanasoma fani za Sayansi na Teknolojia.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimimwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa moja ya tatizo kubwa katika sekta ta madini ni kutokuwa na wataalam waliobobea wa Kizalendo Watanzania katika fani ya utafiti na hivyo kuipelekea Serikali kutegemea zaidi ripoti za wataalam wa kigeni ili kutoa taarifa sahihi za utafiti. Je, Serikali ina mikakati gania kutoa taarifa sahihi za utafiti? Na pili Je, Serikali ina mikakati gani hii Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini ili kuandaa wataalam watakaoweza kufanya kwa karibu katika sehemu za utafiti wa mali hizi tulizo nazo za madini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba hatuna wataalam wa kutafiti. Kwa sababu hawa wawekezaji wakubwa wanaokuja kuwekeza wakubwa hata kwa wadogo wanafuata ile dira ambayo tayari imeshawekwa na wataalam wetu na kituo hicho ambacho kinafanya kazi hiyo. Kituo hicho kiko hapa Dodoma. *Geological Survey of Tanzania*. Kina ramani ya madini yote hapa Tanzania. Sasa kuna tofauti kati ya kujua madini yako wapi na uhakiki wa madini yapo kiasi gani. Kuhakiki madini yapo kiasi gani unahitaji rasilimali kubwa sana ambayo sisi hatutegemei kwamba hiyo *Geological Survey of Tanzania* inataka kutengeneza mgodi. Kwa hiyo, yenyewe inajua kwamba hapa kuna dhahabu, hapa kuna rubi; sasa wewe kama ukitaka

kujua kiasi gani kipo kama kinaweza kufaa kwa uzalishaji wa faida ndiyo unawekeza kusudi ufanye hivyo. Kwa hiyo, utaalam huo upo hapa Tanzania na vijana wetu wanafanya kazi hiyo vizuri. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na pamoja na kuwa Serikali imejitahidi sana bado wasichana wengi wamekuwa woga kuchukua masomo ya sayansi. Pamoja na jitihada hizo kwa kuwa kuna nchi nyingine zimeamua kabisa kufuta ada kwa wasichana ili waweze kusoma. Je, Serikali yetu inaonaje umuhimu wa sisi pia kuiga kutoa ada kwa ajili ya wasichana wetu ili waweze kusoma?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, tunampongeza kwanza Mheshimiwa Janet Kahama kwa kuwafikiria watoto wa kike ili waweze kupata elimu hii ya juu hasa katika masomo ya sayansi. Wizara yangu haijafikiria kufuta ada kwa watoto wa kike lakini imefanya mipango mahususi kwa mfano katika vyuo vya ufundi tuna kozi inatwa *Access Course* na vyuo vikuu tuna kozi inaitwa *Pre-entry course* ambazo ni kozi zinawapendelea wasichana wale ambao hawakufaulu sana masomo ya sayansi walipokuwa *form six*; lakini tukifikiria kwamba huenda kulikuwa na matatizo yaliyowasababisa wasifaulu kama wavulana basi nawachukua na kuwapa hizo kozi katika masomo yale ambayo wamefaulu kiasi. Wanapokuwa wamefaulu wanapewa mtihani baada ya miezi na wakifaulu wanaruhusiwa na wanadahiliwa katika vyuo vikuu; na kozi hizi zimesaidia kuwaingiza wasichana wengi sana katika vyuo vikuu kwa masomo ya sayansi, *engineering* na masomo ya ufundi. Kwa hiyo, nafikiri hizo ni juhudi ambazo tunaendelea kuzifanya na tutaendelea kufanya hivyo. Lakini pia Wizara yangu inatembelea shule za sekondari kila mwaka kuangalia na kushawishi watoto wa kike wajiunge na masomo ya sayansi. Sasa nawaomba wenzangu Waheshimiwa Wabunge sisi wote tuendelee kuwahimiza watoto wa kike wachukue masomo haya na kama mnavyosema ni kweli sio wengi katika masomo. Lakini Wizara inafanya juhudi hizo lakini suala la ada hilo hatuwezi kulifanya sasa hivi.

**Na. 9**

**Gereza la Kilimo – Liwale**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Liwale ina Gereza la Kilimo lililoko katika eneo lililotokana na mashamba ya korosho ya baadhi ya wananchi wa Liwale; na kwa kuwa wananchi hao hawajapata fidia waliyoahidiwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa hiyo kwa wananchi husika?

(b) Kwa kuwa azma ya Serikali ni kulifanya gereza hilo kuwa la kilimo. Je, ni hatua gani zimechukuliwa kuboresha nyenzo husika kama trekta, gari, wataalam na kadhilika?

(c) Kwa kuwa baadhi ya majengo ya gereza hilo lililoanzishwa zaidi ya miaka ishirini (20) iliyopita siyo ya kudumu hasa ofisi na nyumba za askari. Je Serikali ina utaratibu gani wa kujenga nyumba za kudumu katika gereza hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye vifungu vidogo (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza linasubiri wathamini wa Halimashauri ya Wilaya ya Liwale wafanye uthamini unaotakiwa kwa wananchi wanaostahili kulipwa fidia. Kazi hiyo ikikamilika na thamani ikajulikana, Serikali itahakikisha kuwa wananchi wanaohusika watalipwa fidia kwa kadiri wanavyostahili.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inafanya tathimini ya kina ili kubaini magareza machache ya kuyapa kipaumbele. Tathimini ikikamilika matrekta yatanunuliwa na yatapelekwa kwanza kwenye magereza hayo yenye mashamba makubwa. Imeamuliwa, inafaa kuweka nguvu za kutosha kwa maana ya vifaa na fedha kwenye magereza machache kuliko kusambaza kdogo kidogo.Mheshimiwa Spika Liwale kuna gari moja aina ya *KIA* ambalo ni bovu. Hata hivyo Serikali inaendelea na utaratibu wa kununua magari madogo (*pick-ups)* kila mwaka kwa ajili ya Magereza ya Wilaya. Gereza la Liwale ni mojawapo ya Magereza yatakayopata gari mara yatakaponunuliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilitoa fedha za kukamilisha ujenzi wa mabweni mapya ya kudumu miwili ya wafungwa ambayo sasa yanatumika. Mwaka huu 2007/2008 Serikali imetenga Tzs 8,000,000/= kwa ajili ya kufanya utafiti na kuchimba kisima kirefu cha maji safi na salama. Ujenzi wa nyumba za kudumu utaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO**: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Labda tu ningependa kuelewa mnangojea mawasiliano kutoka Halmashauri ya kwamba hadi leo hii gereza hilo lina umri wa miaka 20 na kwamba mawasiliano kati ya magereza pamoja na wananchi wa eneo lile ambalo limechukuliwa kwa ajili ya magereza yameshafanywa kwa siku za nyuma hata kabla ya mimi sijawa Mbunge, wakaahidiwa watalipwa. Hadi hii leo hawajalipwa bado mnasema kuna mawasiliano; naweza nikapata nakala ya mawasiliano hayo ili niweze kuhimiza Halmashauri itekeleze haraka iwezekanavyo?

La Pili, kwa vile gereza la Liwale lipo katika eneo la Serou pia na kwa kuwa kuna wafungwa ambao wamefungwa kwa mujibu wa taratibu za Sheria haoni kwamba kama

majumba ya kudumu yatachelewa kujengwa wataathirika sio askari magereza peke yao pamoja na wafungwa ambao wanaweza kujeruhiwa. Kwa hiyo, wakawa na adhabu mbili, za kujeruhiwa na wanyamapori na pia kufungwa. Sasa hili likoje ningependa kipaumbele kitolewe katika maeneo kama hayo kwa kuwa wapo hatarini watumishi wao wenyewe na wale wafungwa. Tafadhali sana naomba jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mawasiliano yanaendelea na namkaribisha ofisini kwangu ili nimpatie nakala ya mawasiliano hayo ili tuendelee kufuatilia kwa pamoja ili wananchi wa Liwale wafidiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa mabweni ya kudumu kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi. Mwaka wa fedha uliopita tumejenga mabweni mawili na tunaendelea kujenga mabweni na makazi kwa ajili ya askari magereza kadiri jinsi fedha zitakavyopatikana.

Na.10

**Sifa na Taratibu za Kujiunga na Vyombo vya Ulinzi**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa mchakato wa uchujaji wa vijana wanaojiunga na vyombo vya ulinzi umekuwa na urasimu mkubwa unaopelekea malalamiko katika jamii:-

(a) Je, ni utaratibu na sifa gani zinatumika kuwapata vijana hao?

(b) Je, ni nini wajibu wa viongozi wa ngazi mbalimbali katika mchakato wa uchujaji ili kuhakikisha wenye haki ndio wanafanikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kujiunga na chombo chochote kile ni dhahiri kutakuwa na sifa zitahitajika. Kwa upande wa vyombo vya Ulinzi, sifa zinazohitajika wakati wa kujiunga ni kama zifuatazo:-

(i) Mwombaji awe raia wa Tanzania.

(ii) Awe na umri kati ya miaka 18 – 23 kwa askari wa kawaida na kwa wataalam miaka 18-30.

(iii) Awe hajaolewa au kuoa na asiwe amezaa.

(iv) Awe na tabia na nidhamu nzuri hajapatikana na hatia mahakamani na hajawahi kufungwa.

(v) Awe na elimu ya kidato cha IV (kwa askari wa kawaida na kwa wataalam awe na Stashahada ya juu na kuendelea.

Aidha vyeti halisi vitahitajika ili kuthibitisha umri, uraia wake na masomo yake.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kuwapata vijana kujiunga na vyombo vya ulinzi ni kama zifuatazo:-

Makao Makuu ya Jeshi hutuma nafasi kwa kila Wilaya kupitia mkoani. Kamati za ulinzi na usalama za Wilaya hufanya kazi ya kuchambua vijana wote waliopeleka maombi yao kwa kuzingatia sifa za kila mwombaji.

Uchambuzi katika ngazi ya Wilaya unapokamilika orodha hiyo hupelekwa Mkoani ili Kamati za ulinzi na usalama za Mikoa zihakikishe zaidi. Kamati za ulinzi na usalama za Mikoa zinapokamilisha kazi hiyo Kamati za kuandikisha askari wapya kutoka Makao Makuu ya Jeshi, huenda mikoani kukamilisha kazi ya uandikishaji ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa afya za vijana walioteuliwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu mwingine unaotumika sambamba na ule wa kwanza ni kuchukua vijana wenye sifa kutoka Jeshi la Kujenga Taifa moja kwa moja. Kwa upande wa wataalam mchakato wa kuwapata vijana hufanywa moja kwa moja na Makao Makuu ya Jeshi bada ya kupitia maombi ya walioomba.

(b) Mheshimiwa Spika, haki ya kujiunga na vyombo vya ulinzi ni ya kila Mtanzania mwenye sifa zilizoainishwa na vyombo vya ulinzi. Hata hivyo, wajibu wa viongozi wa ngazi mbalimbali katika mchakato wa kuwapata vijana ni kuhakikisha kuwa uchaguzi wao unazingatia sifa na sio vinginevyo.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize swali la nyongeza. Je, ikigundulika vijana waliotumia majina na vyeti bandia. Je, ni hatua gani zitachukuliwa dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ikigundulika kijana yoyote yule kijiunga kwake kumetokana na kutumia vyeti bandia, hatua itakayochukuliwa ni kufukuzwa mara moja.

**Na. 11**

**Suala la Amani na Utulivu Nchini.**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni mhimili wa amani na utulivu.

(a) Je, Visiwa vya Zanzibar na Pemba viko katika hatari kiasi gani dhidi ya magaidi duniani?

(b) Je, Jeshi la Tanzania lina mpango gani wa kuboresha na kuimarisha vifaa vya kivita ikiwa ni utayari wa kuilinda nchi dhidi ya maadui wa karibu na wa mbali, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa manowari za kivita, ndege za kivita *(attack helicopters)* pamoja na vifaru vya kivita.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ugaidi unaoendelea duniani unaonekana kutokuwa na mipaka kutokana na kuwepo kwa mtandao wake sehemu nyingi duniani.

Kwa maana hiyo vitendo vya kigaidi vinaweza kutokea nchi yoyote ikiwa ni pamoja na visiwa vya Zanzibar wakati wowote. Hata hivyo visiwa vya Zanzibar haviko katika hatari dhidi ya magaidi duniani ukilinganisha na sehemu nyingi duniani. Hii ni kutokana na kwamba vitendo vya kigaidi hufanyika maeneo ambayo magaidi wana malengo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatilia maanani suala zima la ulinzi wa nchi dhidi ya maadui. Katika kufanya hivyo Jeshi la Wananchi limepatiwa mafunzo ya kijeshi, vifaa na zana za kisasa ili kulifanya liwe imara zaidi.

Aidha Wizara ya Ulinizi imeandaa mipango wa maendeleo ya Jeshi, wa muda mfupi, wa kati, na muda mrefu ambao unalenga katika kuboresha na kuimarisha zaidi Jeshi. Mpango huo umezingatia pia ununuzi wa zana na vifaa mbalimbali vya kisiasa.

Na. 12

**Kufutwa kwa SHIHATA**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, haki ya kupata habari na kutoa habari ni ya msingi kwa kila Mtanzania; na kwa kuwa, katika Dunia ya Utandawazi Mashirika ya Habari ni ya Kitaifa *(News Agencies)* katika nchi zinazoendelea ndiyo yanayofanya kazi za kukusanya na kusambaza habari nchini kuanzia ngazi za vijiji hadi Taifa na kwa kuwa Tanzania ilisitisha kazi za Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA), hivyo kuifanya nchi yetu kuwa nchi pekee katika Afrika Mashariki na katika *SADC*, isiyokuwa na Shirika lake la Habari la Kitaifa:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha kuifuta SHIHATA licha ya umuhimu wake kwa ustawi na maendeleo ya nchi?

(b) Je, ni Taasisi/Idara gani ilipewa majukumu yaliyokuwa yakifanywa na SHIHATA; kama hakuna, kwa kuzingatia umuhimu wake katika Taifa. Je, ni lini Serikali imepanga kuanzisha tena SHIHATA?

(c) Je, ni nini hasa kazi na wajibu wa maelezo na uhusiano kati ya Idara hiyo na Kurugenzi ya Mawasiliano - Ikulu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mwaka 1992 Serikali iliteua Tume iliyoongozwa na Jaji Mkuu Marehemu Francis Nyalali kutafuta maoni ya wananchi kuhusu mfumo bora wa siasa hapa nchini. Pamoja na mambo mengine. Tume hiyo ilipendekeza sheria iliyoanzisha SHIHATA ifanyiwe marekebisho ili kuondoa ukiritimba wa SHIHATA na hivyo kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari wa kukusanya na kutangaza habari bila kuingiliwa na Serikali au taasisi zake.

Kama sehemu ya utekelezaji iliandaa Muswada wa Sheria wa kufuta Kisheria iliyoitwa – *The Tanzania News Agency (reading) Act No. 7 of 200*0. Muswada huu wa sheria ulipitishwa na Bunge kuwa Sheria mwezi Aprili, 2000. Wakati huo huo

kuhamisha baadhi ya majukumu na kazi za SHIHATA kwenda Idara ya Habari – MAELEZO.

(b) Baada ya Serikali kulifuta Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA), majukumu yake yalihamishiwa Idara ya Habari (MAELEZO) ambayo ni msemaji mkuu wa Serikali kuhusu sera na Mipango ya Serikali kwa mujibu wa kifungu cha Sheria Na. 16 (*Standing Order C. 16)* kilichoanzisha Idara hiyo. Serikali haina mpango wa kuanzisha tena SHIHATA. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, Serikali itaendelea kuhamasisha Sekta binafsi ya habari kuanzisha mashirika yao ya habari iwapo zitaona umuhimu wa kuwa na mashirika yao.

(c) Idara ya Habari (MAELEZO) ni sehemu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kazi zake kuu ni pamoja na:-

% Kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali kuhusu sera na mipango ya Serikali *(Standing Order C.16);*

% Kukusanya na kusambaza habari na picha kuhusu shughuli za Serikali na miradi ya maendeleo kote nchini (*The Tanzania News Agency (Repealing Act) No. 7 of 2000);*

% Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji;

% Kuratibu Sekta ya Habari na vyombo vya habari Kitaifa;

% Kuwa mamlaka ya usajili wa magazeti na majarida;

% Kuratibu shughuli za vitengo vya habari na mawasiliano vya Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali.

Kurugenzi ya Mawasiliano Ukulu ni sehemu ya Ofisi binafsi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zake kuu ni:-

% Kuwa Msemaji wa Rais;

% Kuratibu mambo ya habari kuhusu shughuli za Rais;

% Kusimamia Maktaba ya Ikulu.

Mheshimiwa Spika, uhusiano uliopo kati ya Idara ya Habari (MAELEZO) na Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu ni kwamba, hizi zote ni Idara za Serikali zinazofanya kazi za kuratibu shughuli za habari za kila siku.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wakati SHIHATA inavunjwa mwaka 2000 tayari ilikuwa

na mtandao mkubwa ambao ulikuwa umeenea katika nchi nzima hivyo kukidhi mahitaji na matarajio ya wananchi.

Je, Serikali inaweza kusema Idara ya Habari Maelezo ina mtandao nchi nzima na kama mtandao wake uko katika baadhi ya mkoa, pale ambapo Idara ya Habari Maelezo haina ofisi ni Idara gani hufanya kazi ya kukusanya habari na picha zinazohusu masuala ya Serikali na athari zake kwa taifa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati huo SHIHATA ilikuwa na mtandao nchi nzima lakini kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba shughuli zilizokuwa za SHIHATA sasa nyingine zimehamishiwa MAELEZO lakini pia tangu mwaka 2000 Mashirika mengi ya habari binafsi yameibuka katika nchi yetu na kufanya kazi kama zilizokuwa zinafanywa na SHIHATA wakati huo. Kwa hiyo, suala zima la kwamba Idara ya Maelezo haina mtandao nchi nzima inakuwa haina nguvu sana kwa sababu mashirika mengi binafsi yametambaa karibu nchi nzima.

Lakini zaidi ya hapo katika yale maeneo ambayo Idara ya Maelezo haina mtandao wake kuna mawakala wa habari ambao wanafanya kazi hiyo na kupeleka habari zao Maelezo lakini pia bado wanatumika kwa vyombo vingine vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Habari ya mwaka 2003 suala kwamba kuna athari za habari katika nchi yetu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lembeli na Bunge lako Tukufu kwamba kwa kweli athari hizo hazipo na vyombo vya umma tunazidi kuviimarisha siku hadi siku na suala zima la habari linazidi kuchukua sura mpya.

Na. 13

**Kutosikika kwa RTD na Kutoonekana kwa TVT**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi hupenda kusikiliza *Radio Tanzania* na kwa kuwa taarifa muhimu za kitaifa na Kimataifa na kwa kuwa usikivu wa *Radio* hiyo ni hafifu katika sehemu mbalimbali mkoani Manyara ikiwemo Babati ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa na kwa kuwa pia TVT haionekani bila ungo ambao ni ghali:-

(a) Je, ni sababu zipi zinafanya usikivu wa *RTD* kuwa wenye kiwango cha chini katika maeneo yaliyotajwa?

(b) Je Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma ya TVT Babati na Mkoa wa Manyara kwa kuweka vituo/mitambo itakayowezesha wananchi kuona TVT bila kutumia ungo kama ilivyo kwa sehemu nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge wa Babati, kwamba matangazo ya *Radio Tanzania* katika Mkoa wa Manyara na Mji wa Babati usikivu wake ni hafifu. Hii inasababishwa na mitambo ya kurusha matangazo iliyopo katika Mkoa wa Dodoma na Arusha kuwa katika hali ya uchakavu hivyo kushindwa kurusha matangazo wakati wote katika Mkoa wa Manyara na Mji wa Babati.

(b) Mheshimiwa Spika Serikali inakusudia kufunga mitambo ya Televisheni katika Mkoa wa Manyara fedha zitakapopatikana. Hii itakwenda sambamba na Mikoa mingine ya Ruvuma, Iringa, Morogoro, Kilimanjaro, Singida, Shinyanga na Rukwa kwa awamu ya kwanza. Baada ya hatua hiyo wananchi wa Manyara na Mikoa hiyo mingine wataanza kuona Televisheni bila kuhitaji kutumia ungo katika maeneo yao. *(Makofi)*

**MHE. OMARY S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. Vile vile nimshukuru Naibu Waziri kwa kueleza hali halisi inayowafanya wananchi wa Babati washindwe kupata usikivu mzuri wa Redio Tanzania. Kwa hilo, nashukuru sana.

Sasa, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, hali hii ya usikivu hafifu wa Redio Tanzania itakwisha lini kwa mji wa Babati na Mkoa wa Manyara kwa ujumla?

La pili, Serikali imesema inakusudia kufunga mitambo ya Televisheni katika Mkoa wa Manyara na kwamba hii itasaidia vile vile na Mikoa mingine. Sasa kwa sababu kufunga mitambo kunaendana na bajeti au upatikanaji wa fedha, je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha ujao fungu hilo linatengwa ili wananchi wa Babati na Mikoa iliyotajwa waweze kuona TVT bila kutumia ungo? Asante!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, la kwanza linalohusu usikivu huu utaisha lini katika Mkoa wa Manyara na Mji wa Babati, niseme tu kwamba, kwa kweli tatizo kubwa tulilonalo sisi ni fedha katika sekta hii. Mkakati wetu, matarajio mengi ni kwamba mwaka ujao wa fedha hali ya fedha ikiwa nzuri, sekta yetu ya habari itapewa kipaumbele ili Mikoa kama ya Manyara na Mji wa Babati iweze kupata usikivu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Kwaangw' avute subira kidogo, tuone hali itakuwaje mwaka ujao wa fedha. *Inshallah*, mambo yakiwa mazuri tutapata fedha na tutaweza kuingiza katika bajeti yetu kuweza kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza na la pili, yanafanana, vyote vinategemea fedha. Mtambo mmoja wa kurusha matangazo ya televisheni gharama yake ni takribani milioni 900. *Again*, ni matarajio yetu mwaka ujao wa fedha, hali ya uchumi ikiwa nzuri, ni kwamba sasa sekta yetu ya habari itapewa kipaumbele na tutaweza kufunga mitambo hiyo katika miji niliyoitaja pamoja na Mji wa Babati na Mkoa wa Manyara.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Matangazo, wageni wetu Bungeni leo, kwanza wageni wa Mheshimiwa Wilson Masilingi ambao ni Ndugu Marystella Masilingi, ni Mkewe Mheshimiwa Mbunge. Naomba asimame pale alipo. Karibu sana. Pamoja naye yupo Bwana Venant Masilingi, kaka yake Mheshimiwa Mbunge na pia wameambatana na shemejie na baadhi ya wapiga kura wake; Ndugu Makopa, Ndugu Bayonga na Ndugu Kakobe. Naona ndiyo wale wamesimama pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, anao wageni wake ambao ni Ndugu Abdallah Rashid Abdallah, yule pale ambaye ni shemeji yake lakini pia ni mshauri wa Rais wa Zanzibar,  Kilimo, Mazingira na Umwagiliaji. Inaelekea, sijui Mheshimiwa Mwinchoum ameoa Zanzibar au basi sawa nchi hii ni moja, sawa tu! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mohamed Rajab, anakumbusha wanamichezo wote Wabunge kwamba mazoezi yataendelea kesho asubuhi kama kawaida kwenye uwanja wa Jamhuri na magari yapo kama kawaida kwa huduma hiyo.

Mheshimiwa Omary Kwaangw', Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii, ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii, leo tarehe 30 Oktoba, 2007, saa 04.30 asubuhi katika ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, nataka mfahamu tu kwamba, kwa sasa hivi wakati Kiongozi wa Shughuli za Upinzani akiwa India kwa matibabu, basi Kiongozi wa Upinzani anayekaimu ni Mheshimiwa Dr. Wibrod Slaa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la pili, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu kusimamishwa kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Kabwe Zitto. Jambo hili limekuwa likiandikwa andikwa hasa kwenye magazeti na kukuzwa. Lakini, Mheshimiwa yule amesimamishwa chini ya Kanuni ya 61 na ni wajibu wa Mbunge yeyote kutii Kanuni tu. Kwa hiyo, nisome Kanuni ya 61 kwa sababu ya kuliweka wazi jambo hili:

"Mbunge aliyesimamishwa kazi kwa mujibu wa Kanuni ya 59(3) na 60(2), atatoka katika Bunge na hataingia tena katika sehemu yoyote ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge kwa muda wote atakapokuwa amesimamishwa na atalipwa nusu mshahara na nusu posho zozote zinazoambatana na mshahara huo".

Sasa hoja kwamba adhabu haikamiliki mpaka aandikiwe barua, ni hoja potofu. Hakuna utaratibu wa namna hiyo. Kila Mbunge anatakiwa atii Kanuni hizi. Ikishatamkwa kwa mujibu wa Kanuni, ndiyo amri yenyewe hiyo, ndiyo taarifa yenyewe!

Pia nifafanue zaidi kwamba, kwa hiyo adhabu hii ya kusimamishwa kwa Mheshimiwa huyo, inaisha tarehe 16 Novemba, 2007. Kuanzia asubuhi ya tarehe 17 Novemba, atashiriki katika Kamati, katika shughuli zote za Bunge pamoja na Mheshimiwa Spika kuweza kumtumia kwa kazi yoyote ambayo ataona itafaa. Kwa hiyo, mara ya mwisho nilipotamka kwamba ataingia Bungeni Januari, maana yake ni kushiriki katika Mkutano wa 10. Lakini, adhabu hii inaishia tarehe 16 Novemba, 2007 ambapo ndiyo mwisho wa Mkutano wa Pili kwa maana ya adhabu ile. Kwa hiyo, kuanzia tarehe 17, Novemba, 2007 atakuwa huru kuweza kushughulika bila vikwazo vilivyopo kwenye Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao walikuwa hawajatambua hivyo, nilikuwa napenda niwafahamishe kwamba Mheshimiwa Spika leo kavaa Joho Jipya kwa sababu Joho nililokuwa natumia lina umri wa miaka 12 na wengine mlikuwa mkiniandikia kwamba rangi zimeanza kufifia. Bado litaweza kutumika, lakini tuliona si vizuri kuendelea na Joho chakavu. Kwa taarifa yenu tu, Joho si kitu cha hovyo hovyo kwa sababu nyuzi zake ni nyuzi za dhahabu. Ndiyo! Linachukua miezi kadhaa kushonwa. Darizi yake, inafanyika Uingereza, kule London kwa kutumia nyuzi za dhahabu. Kwa hiyo, si kitu rahisi. Bahati njema kwa nchi ni kwamba halichakai hadi miaka kuanzia 12 hadi 15. Kwa hiyo, halinunuliwi kila mara. Niliona mfahamu hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho, Waheshimiwa Wabunge, nina majukumu mengine, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Spika aongoze shughuli. Ala! Amekwishaingia! *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Asalaam *Aleikhum*! Aha, mimi ni lile lile. *(Kicheko)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007 *(The Public Service (Amendment) Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge kama mnavyojua, maombi ya kuchangia tunaona tuna Mbunge mmoja. Kwa hiyo, yanakaribishwa maombi ya kuchangia. Tuna Mbunge mmoja tu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa hoja yangu, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini, kutoa salaam za rambi rambi kwa familia ya marehemu, Mheshimiwa Salome Mbatia aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambaye alifariki Dunia tarehe 24/10/2007 siku ya Jumatano huko Kibena, Iringa kwa ajali mbaya ya gari. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa faraja familia ya marehemu na Mungu ampumzishe mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa ruhusa yako, naomba kuwapa pole wananchi na familia ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM, Urambo ambaye alipata ajali ya gari na baadaye kufariki dunia siku ya tarehe 27/10/2007. Pia namwombea yeye pamoja na Askari wawili waliofariki awali kwa ajali hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kuwapa pole na kuwatakia bhukheri wa afya na matibabu mema Mheshimiwa Mudhihiri Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga ambaye alipata ajali ya gari huko Lindi iliyosababisha akatwe mkono na Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye naye alipata ajali ya gari huko Urambo, Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nimtakie afya njema na matibabu mema Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambaye amelazwa katika Hospitali ya Hindu Mandal, Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninawapa pole ndugu na jamaa wote walioondokewa na ndugu zao katika kipindi hiki katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam hizo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwaka *2007 (The Public Service (Amendment) Bill, 2007)* sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Na.8 ya Mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Utumishi wa Umma inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho, ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo tarehe 12 Aprili, 2002 na utekelezaji wake ulianza tarehe 1 Julai, 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ilitungwa mahsusi kama nyenzo ya kutekeleza misingi ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1998. Misingi muhimu ya sera hii ni kujenga utumishi ulio imara kwa kuwa na mifumo ya menejimenti inayolenga kupata matokeo *(result oriented management)* na mifumo iliyowazi katika ajira, nidhamu, kupandishwa vyeo na kupimwa utendaji wa kazi. Sheria hii pia inalenga kupeleka mamlaka ya usimamizi wa watumishi katika sehemu zao za kazi *(decentralization)* kwa kuwapa madaraka zaidi watendaji wakuu. Mifumo hii inalenga kuiwezesha Serikali kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoonyesha hapo awali, sasa ni mwaka wa tano tangu sheria hii ilipoanza kutumika. Pamoja na malengo mazuri yaliyokusudiwa, kumekuwepo upungufu katika utekelezaji wa baadhi ya vipengele kwa baadhi ya vifungu vya sheria hii. Upungufu ulijitokeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ya nchi ambayo yameshindwa kuwavutia waombaji wa kazi wenye sifa zinazotakiwa hususan Mikoa ya pembezoni.

Watendaji kutumia muda mwingi kutangaza na kusaili waombaji wa kazi.

Utaratibu wa ajira kuwa mrefu na hivyo kufanya baadhi ya nafasi kuwa wazi kwa muda mrefu.

Baadhi ya watumishi kutotaka mabadiliko na hasa kutoukubali mfumo wa kupima utendaji wao kwa uwazi *(OPRAS)*.

Sheria kujumuisha baadhi ya makundi ya watumishi wa umma ambayo kwa asili ya utendaji wake wa kazi yanahitaji taratibu tofauti za uendeshaji kama vile; watumishi wa huduma za Zimamoto, Uokoaji na Uhamiaji.

Baadhi ya watumishi wanaoajiriwa kutoka katika soko la ajira kutumia muda mwingi kujifunza taratibu za uendeshaji wa kazi za Serikali hivyo kuvuruga utamaduni wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kurekebisha kasoro hizo na kuweka vifungu vya kuboresha utendaji kazi bila kuathiri misingi ya sera ya menejimenti na ajira katika utumishi wa umma. Marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kukidhi mabadiliko yanayotokea na yanayoendelea kutokea katika utumishi wa umma na kuondoa upungufu uliojitokeza. Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mamlaka ya Ajira katika Wizara kwa watumishi wote kuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara husika. Hilo, limetekelezwa kwa kuondoa vifungu vinavyomtaja Mkurungenzi wa Idara kuwa ni Mamlaka ya Ajira kwa watumishi wa Huduma za Kawaida *(Operational Services)*

- Sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma itaundwa ikiwa ni pamoja na kubainisha kazi zake.

Kutoa ufafanuzi kuhusu uhamisho wa watumishi wa umma kutoka sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine pale inapobidi au kwa maslahi ya umma.

Kurekebisha kazi za Tume ya Utumishi wa Umma kutoka Tume Tendaji na kuwa Tume Rekebu.

Mishahara na marupurupu mengine ya wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma kupangwa na Katibu Mkuu Kiongozi badala ya Katibu Mkuu Utumishi.

Wakala za Serikali kutawaliwa pia na Sheria ya Utumishi wa Umma, Na. 8 ya mwaka 2002.

Watumishi wa Idara ya Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji kuondolewa katika Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kuweka taratibu bora za kushughulikia masuala ya watumishi wa umma .

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una vifungu 14. Kifungu cha kwanza kinahusu masuala ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa pamoja na uhusiano wake ana sheria mama. Kifungu cha pili, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 5 cha sheria ambacho kitafuta kifungu kinachohusu Uhamiaji na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji katika kundi la watumishi wa umma wanaosimamiwa na sheria hii. Kifungu cha tatu, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 6 cha sheria mama kwa kuongeza kifungu kinachosimamia utendaji kazi wenye matokeo na upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma kwa utaratibu wa *OPRAS*. Kifungu cha nne, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 7 cha sheria mama. Marekebisho haya yanadhamiria kuondoa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Kifungu cha tano, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 8 cha sheria mama kwa kuondoa kifungu cha 8(3)(f) na kukifanyia marekebisho yanayoainisha taratibu za uhamisho katika Utumishi wa Umma, jambo ambalo hapo awali halikuainishwa katika sheria inayorekebishwa. Aidha, kifungu hiki kinazipa nguvu za kisheria nyaraka za Utumishi ambazo hutolewa mara kwa mara kutekeleza utekelezaji wa mambo mbali mbali chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha sita, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 9(3) cha sheria mama kwa kuondoa kifungu 9(3)(v) kinachohusu Uhamiaji na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji. Kifungu cha saba kinahusu marekebisho ya kifungu cha 10 cha sheria mama. Kifungu hiki kinaondoa kifungu cha 10(c) na (d) ili kuipa Tume ya Utumishi wa Umma uwezo wa kuwa Tume Rekebu na siyo Tume Tendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha nane, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 12 kinachoainisha utaratibu wa upangaji wa mishahara na marupuru ya wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma ili kupangiwa mishahara na marupurupu yao na Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Katibu wa Utumishi. Kifungu cha tisa, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 15 cha sheria mama, dhamira ikiwa ni kuondoa kifungu cha 15(d) kinachohusu Idara ya Zimamoto na Uokoaji katika

sheria inayorekebishwa. Kifungu cha kumi, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 25 cha sheria mama kinachomhusu Mkurugenzi wa Uhamiaji, Idara ya Zimamoto na Uokoaji. Aidha, kifungu cha kumi na moja, kinahusu marekebisho yanayoingiza kifungu kipya cha 29 kinachohusu uundaji wa Sekretarieti ya Ajira *(Public Service Recruitment Secretariat)* chombo ambacho ndicho kitasimamia na kuratibu mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma. Chombo hiki ndicho kitakachotangaza nafasi za kazi kwa niaba ya mamlaka mbali mbali za ajira, kitasaili waombaji na hatimaye kuwasilisha waombaji waliofaulu kwenye mamlaka za ajira ili kukamilisha mchakato wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha kumi na mbili, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 30 cha sheria mama. Marekebisho haya yanakusudia kuwataka Wakala wa Serikali kutawaliwa pia na sheria ya Utumishi wa Umma. Kifungu cha kumi na tatu, kinahusu marekebisho ya kifungu cha 34 cha sheria mama kinachoongeza sehemu ya (f) ambayo itaampa Waziri uwezo wa kutengeneza kanuni zitakazosimamia taratibu za uhamisho wa watumishi wa umma. Kifungu cha kumi na nne, kinahusu utayarishaji wa kanuni na miongozo ya utekelezaji wa masuala mbali mbali katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, mapendekezo niliyoyawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba niwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora chini ya uongozi thabiti wa Mwenyekiti, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kwa michango yao waliyoitoa kwa lengo la kuboresha Muswada huu. Kutokana na umakini na michango ya Kamati hii, imewezesha kazi ya kuwasilisha Muswada huu kufanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wajadili mapendekezo yaliyomo katika Muswada huu na hatimaye kupitisha na kuwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma *(The Public Service (Amendment) Act, 2007)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007 *(The Public Service (Amendment) Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpwapwa na kwa niba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba nitoe salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika na kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu na jamaa, kutokana na kifo cha ghafla cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (CCM) na Naibu

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Marehemu Salome Joseph Mbatia, aliyefariki dunia kwa ajali mbaya ya gari iliyotokea tarehe 24 Oktoba, 2007 katika kijiji cha Kibena, Njombe, Mkoa wa Iringa. Aidha, nachukua fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na familia za marehemu wote waliofariki katika ajali hiyo. Vifo vya marehemu hao siyo tu vimeacha pengo kubwa kwa familia zao, bali pia vimelipotezea Taifa watu muhimu ambao bado lilikuwa linawahitaji. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu iliujadili Muswada huu tarehe 22 Oktoba, 2007 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar-es-Salaam. Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb., Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kuhusu marekebisho yaliyokusudiwa. Kama alivyoeleza Mtoa Hoja, Muswada huu unalenga kufanya marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Na.8 ya Mwaka 2002 kutokana na upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili kwa kina, Kamati imeridhika kuwa marekebisho haya ni muhimu na yatasaidia sana kurekebisha dosari zilizojitokeza. Serikali ina kila sababu ya kuleta marekebisho haya kwa kuzingatia kuwa tangu sheria hii itungwe ni miaka minne imepita sasa kuiwezesha kuifanyia tathmini na kuwasilisha marekebisho husika. Kimsingi Kamati inaunga mkono marekebisho yote yaliyopo katika Muswada huu. Aidha, Kamati inaafikiana na pendekezo la Serikali kuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti ateuliwe na Rais kama ilivyoelezwa katika ibara ya 11 ya Muswada inayoanzisha kifungu kipya cha 29 katika Sheria ya Utumishi wa Umma, kinachoanzisha Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma *(Public Service Recruitment Secretariat)*. Pamoja na hayo, kwa kuzingatia kuwa Rais ana majukumu mengi, Kamati inashauri kuwa Mawaziri pia wapewe mamlaka ya kuwateua Wenyeviti wa Bodi au vyombo vingine.kama nilivyosema hapo awali, mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu yamekuja kwa wakati muafaka kulingana na mabadiliko ya wakati. Kwa sababu hiyo, Kamati yangu inaamini kuwa Muswada huu ukipitishwa na Bunge lako Tukufu utasaidia kuboresha sekta ya utumishi wa umma katika maeneo mbalimbali. Mwisho, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha Maoni ya Kamati. Pia namshukuru Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), Katibu Mkuu, Bw. George Yambesi na wataalamu wote wa Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kushirikiana vema na Kamati wakati wa kuujadili Muswada huu. Kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango yao ya kina iliyoboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba niwataje kama ifuatavyo:- Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti; Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Pindi H. Chana; Mheshimiwa Stephen J. Galinoma; Mheshimiwa Athumani S. Janguo; Mheshimiwa Rajab H. Juma; Mheshimiwa Shoka K. Juma; Mheshimiwa Charles N. Keenja; Mheshimiwa John P. Lwanji; Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi; Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno; Mheshimiwa Halima J. Mdee; Mheshimiwa Nimrod E. Mkono; Mheshimiwa Salim Y. Mohammed; Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. Pia nawashukuru Makatibu wa

Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Emmanuel Mpanda, kwa kuihudumia Kamati wakati wote wa Kikao na kutayarisha Maoni ya Kamati mapema. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU – MSEMAJI WA UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Na.43(5)(b) na (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa niba yangu mwenyewe, kutoa salaam za rambi rambi kwa familia, Mheshimiwa Rais, ndugu, Waheshimiwa Wabunge wote na marafiki kwa msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na mpendwa wetu Hayati Salome Mbatia aliyetutoka hivi karibuni katika ajali ya gari. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Naomba kutoa salaam za pole pia kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamekumbwa na mitihani migumu ya Mwenyezi Mungu kama vile kuondokewa na wapendwa wao au waliopata ajali. Naomba Mwenyezi Mungu awape roho ya subira na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu. Pengine sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuchukua hatua madhubuti kuangalia namna makini ya kupunguza kabisa wimbi hili la ajali zisizoisha kila kukicha na kupoteza maisha ya watanzania wengi, viongozi na wananchi katika ujumla wao. Haitoshi kuomboleza na kulalamika kama hatutachukua hatua za dhati na makusudi katika kukabiliana na tatizo hili zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa niaba yangu mwenyewe, kutoa salamu za rambirambi kwa familia, Mheshimiwa Rais, ndugu, Waheshimiwa Wabunge wote na marafiki kwa msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na mpendwa wetu Hayati Salome Mbatia aliyetutoka hivi karibuni katika ajali ya gari. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amin.

Naomba kutoa salamu za pole pia kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamekumbwa na mitihani migumu ya Mwenyezi Mungu kama vile kuondokewa na wapendwa wao au waliopata ajali. Naomba Mwenyezi Mungu awape roho ya subira na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu. Pengine sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuchukua hatua madhubuti kuangalia namna makini ya kupunguza kabisa wimbi hili la ajali zisizoisha kila kukicha na kupoteza maisha ya Watanzania wengi, viongozi na wananchi katika ujumla wao. Haitoshi kuomboleza na kulalamika kama hatutachukua hatua za dhati na makusudi katika kukabiliana na tatizo hili zito.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Hamad Rashid, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambaye alifiwa na mama yake hivi karibuni wakati yeye mwenyewe akiwa India kwa matibabu. Mwenyezi Mungu ampe nguvu na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu. Kwa vile Mheshimiwa Hamad anategemewa kufanyiwa operesheni Jumatano ijayo, tunamwomba Mwenyezi Mungu aweze kumpa nguvu kupokea maumivu yote, amjalie afya tena ili arudi mapema kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza , kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na watendaji wote kwa kuleta marekebisho ya sheria hiyo muhimu kwa watumishi wa umma. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wangu wa kambi Mheshimiwa Hamad Rashid Mbunge wa Wawi, na Mheshimiwa Dr. Slaa Mbunge wa Karatu kwa kutuunganisha katika utendaji wa kazi zetu. Vilevile napenda kuwashukuru Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Shoka Juma na Mheshimiwa Salum Yusuph ambao ni wajumbe katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa msaada wao mkubwa katika uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kambi ya Upinzani inayo maoni machache ambayo tungependa Mheshimiwa Waziri ayatolee ufafanuzi au kuyafanyia kazi kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 3(a) ya Muswada inayofanya marekebisho katika kifungu cha 6(1) kwa kufuta kifungu kidogo cha (a) na kuweka kifungu kipya (a) (i) kinachosomeka, nanukuu: "*Result Oriented Management*", Kambi ya Upinzani inaona kuwa utawala utakaojali zaidi matokeo hautakuwa na tija bila ya kujali mchakato mzima wa kufikia matokeo hayo. Katika Utumishi wa Umma ili tija kupatikana utawala unatakiwa umwangalie mwananchi au mteja kuwa ndiyo kitovu kabla ya matokeo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona ni bora badala ya kuwa na *result oriented management* peke yake iwe pia na *customer oriented management* kwa lengo la kuhuisha utumishi kwa lengo zima la utumishi huo. Utumishi wa umma hauna maana kama hauna lengo la kutoa huduma kwa viwango vya juu kwa wananchi ambao ndiyo walengwa mathalani masuala yote ya lugha, nidhamu kazini na masuala yote ya mkataba kati ya mwajiri na walengwa yaani watumishi. Kwa mfano japo mkataba unataka barua za wananchi ziwe zimepatiwa majibu au angalau maelezo ndani ya siku saba imebaki kuwa ndoto. Hivyo kipengele kinachoongelewa hakitakuwa na tija yeyote iwapo vifungu hivyo havitakuwa na uhusiano na lengo hilo la msingi. Ni kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani inadhani ni vema kuongeza suala la *customer oriented management.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa utawala ukishamuona mwananchi kama mteja katika utendaji mzima wa kazi, utasababisha uwepo wa uwazi katika mapato na mgawanyo mzima wa rasilimali jambo litakaloleta matokeo mazuri katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa suala si matokeo kwani tunaamini matokeo yanaweza yakatengenezwa na kuaminishwa baadhi ya watu kuwa yamefanyika na madhara yakaja kuonekana baadaye wakati wahusika wenyewe hawapo. Mara ngapi taarifa nyingi zimeaandikwa tu mezani na hata siku za hivi karibuni viongozi wa juu wamelalamika kuandikiwa taarifa zisizosahihi. Jambo hili linaweza kusababisha hasara kubwa kwa jamii husika na Taifa kwa ujumla. Ni vema sheria ikakinga madhara haya kwa kiwango kinachowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani pia suala hili linaendana sana na jinsi wafanyakazi wetu wa ngazi mbalimbali wanavyojengewa uwezo, (*capacity building*) lakini pia jinsi wanavyowezeshwa kwa kupatiwa vifaa na nyenzo muhimu za kazi. Mfanyakazi asiye na nyenzo mathalani Bwana Shamba anayewajibika kuzunguka Kata au Tarafa nzima na hana usafiri wa aina yeyote angalau baiskeli itakuwa muujiza kutegemea kuwa atafanya kazi na kupimwa kwa matokeo yaani *results*, hivyo ndilo litakalosababisha taarifa kuandaliwa tu mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 3(b) ambayo imefuta kifungu cha 3 na kuweka kifungu kipya cha 3 kinachotoa mamlaka kwa kila Mkuu wa Idara, *every head of depatment or division,* ni vema kikatoa ufafanuzi wa wazi kuhusu mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mamlaka hizi, nafasi za Baraza la Madiwani hazijawekwa wazi jambo ambalo mara nyingi limeleta mgogoro. Iwapo Mkuu wa Idara kwa maana ya *City Director* bila kuhusisha mamlaka ya kisheria yaani Baraza la Madiwani, sheria hii ni dhahiri inaleta mgongano wa wazi kati ya *DED, City Director* na *Manicipal* Director na mabaraza husika ambayo kisheria ndiyo chombo chenye maamuzi kuhusu masuala yote ya Serikali za Mitaa ikiwemo suala la ajira. Ni vema basi mipaka ya wakuu hao na ya mabaraza ikawekwa wazi na sheria badala ya kuachwa itafisiriwe holela na kuendelea kuleta migongano kama tumedhamiria kupeleka madarakla chini kwa *D by D* basi ni vema katika sheria na taratibu zetu tukaanza kutekeleza sera hizo kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 3(d) ambayo imeweka kifungu kipya cha 6A(1) kinachohusu upatikanaji wa madaraka na ujazwaji wa nafasi za wazi, naomba kunukuu:

"*where a vacancy post occurs in the Service such post shall be filled by suitable employee in the public service ...*"

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua nia nzuri ya kuwafanya watumishi walio katika Wizara, Idara na vyombo vingine vya utumishi wa umma kupanda madaraja ya uongozi. Wasiwasi ni kuwa ndani ya mazoea katika utendaji wa kazi utaendelea kuwepo na jambo hilo ndilo linasababisha Utumishi wa Umma kutokutoa matokeo yanayotegemewa na wananchi kwa kulinganisha sekta binafsi. Kambi ya Upinzani inasisitiza iwapo hilo lazima lifanyike basi isiangaliwe tu muda wa kazi *seniority* bali na *perfomance* yaani utendaji wa kazi wa mhusika na upimwe kwa kigezo cha wazi bila upendeleo wa aina yeyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifungu cha maneno ambacho nimekinukuu hapo juu ni kwamba Serikali inawanyima haki watu wenye sifa za nafasi hiyo lakini hawapo katika Utumishi wa Umma kwani kinatoa umuhimu wa kwanza kwa wale wote waliomo katika sekta ya umma tu na wale wasiokuwemo umuhimu wa pili kama ambavyo katika kifungu hicho kinavyosema ninanukuu:

"*...in the abscence of such employee consideration shall be given to suitable person outside the Service*".

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kuwepo katika sheria za nchi yetu inayoamini kuwa kila raia anastahili fursa na haki sawa ya kushika nafasi yeyote ya kazi na shughuli yeyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi, Ibara 22(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kambi ya Upinzani inaona ni uvunjifu wa Katiba kwa Serikali kuanza kuwabagua raia wake kwa kuwaweka katika madaraja katika utoaji wa fursa za ajira badala ya kutoa haki sawa ya kushindana katika usaili, japokuwa kifungu cha 6A(2) kinasema nafasi zote zinatangazwa na usaili utafanyika. Uzoefu katika nchi yetu unaonesha kuwa nafasi nyingi hata zinazotangazwa tayari kuna mtu analengwa na tangazo ni kisingizio tu cha kutimiza masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza umuhimu wa vigezo uwekwe mbele, sharti ufuatwe kikamilifu na dalili zote za ubaguzi, upendeleo zipigwe vita, haya yasipofanyika sheria itabaki tu vitabuni ndiyo maana Watanzania wengi wanaamini kuwa huwezi kupata kazi bila ya kuwa *referee.* Huu ni wakati muafaka sasa Waziri kuwahakikishia Watanzania wakati anahitimisha ni kwa namna gani atapiga vita mazoea haya na kuondoa kabisa hisia hizi zinazojengwa miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kwani kifungu cha 1,2 kuhusiana na ujazwaji wa nafasi za wazi, cha kwanza kinamnyima haki ya ushindani yule asiyekuwa katika utumishi wa umma, je huo usahili una maana gani? Kama kuna wale walio kwenye utumishi wa umma na wale wasiokuwemo, je ni kweli haki inaweza kutendeka kulingana na vifungu hivyo viwili kwa wale wasiokuwa katika utumishi wa umma?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, kwa kulingana na vigezo vilivyowekwa katika kifungu 6A(3) nafasi zilizo wazi zinawezwa kujazwa kwa vigezo hivyo na ukawepo uhamisho kwa wale waliopata vyeo kwenda katika idara nyingine za Serikali yaani ukawepo na ubadilishanaji toka Wizara moja na nyingine kwa watumishi waliopo katika vyeo vinavyolingana. Kwa njia hii ile dhana ya ufanyaji kazi kwa mazoea miongoni mwa watumishi itapungua kama sio kuondoka kabisa lakini kama hivyo haitowezekana basi haki sawa itendeke kwa mujibu wa Ibara ya 22 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 6A(3)(c) kinachohusu *seniority* kama kigezo kimojawapo cha kupanda cheo, tunaona kuwa kigezo hicho kinawanyima vijana wenye moyo na watendaji kazi wazuri kwa kuwa wana muda mchache katika utumishi na hilo sio haki kwani kuna watumishi wengi wana muda mrefu lakini muda wao kazini hauna muingiliano wa moja kwa moja na ubora wa kazi. Mifano ni mingi tu na zaidi kwa wale wazoefu ni mbinu za kuwakwamisha watendaji wapya ambao wanadhani ni tishio katika ajira zao.Kambi ya Upinzani inaona kigezo hicho kiondolewe kwani unaweza kuwa *senior* lakini hauna *qualification* zinazotakiwa.

Mwisho, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Madiwani wote wa Vyama vya Upinzani waliofanikiwa kushinda nafasi hizo katika chaguzi zilizofanyika siku ya Jumapili. Nasema karibuni katika kujenga demokrasia ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema kuna nafasi ya wachangiaji kama watu wanataka kuchangia na mpaka sasa nina jina moja tu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kabisa niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia, naomba kwanza niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa msiba mkubwa uliotupata wa mpendwa wetu Mheshimiwa Salome Mbatia aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambaye tumekaa naye, tumefanya naye kazi kwa muda mrefu, tunamfahamu jinsi alivyokuwa mchapa kazi lakini Mwenyezi Mungu naye ana mipango yake. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe pole kwa wale wote ambao wamepata majanga mbalimbali hasa ajali au maumivu kwa magonjwa akiwemo Mheshimiwa Mudhihir na pia Kiongozi wangu wa Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid. Mwenyezi Mungu awape nguvu kuweza kurudi kuungana na kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwanza Mswada huu umekuja wakati mzuri. Ni Muswada muhimu na nadhani utendaji kazi katika nchi unategemea sana watumishi wa umma. Kama watumishi wa umma hawako katika mazingira mazuri basi kazi zote tunazofanya, mipango yote tunayopanga, maendeleo yote tunayopanga hayawezi kutekelezeka kwa sababu watumishi wetu wa umma wana matatizo au kuna dosari au kuna kasoro katika sheria au katika taratibu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani nikubaliane na mawazo yaliyotolewa na Waziri na Mwenyekiti wa Kamati na Kiongozi wetu msomaji wetu Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba Muswada umekuja katika wakati muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukazia mambo machache tu. La kwanza, ni hili suala la *result oriented.* Naomba niungane na haitatosha ni vema tukaongeza vilevile *customer oriented.* Ninalisema hili kwa sababu katika sayansi ya *management* ya kisasa dhana kubwa inayotumika sasa ni dhana ya kumwona mhudumiwa mwananchi katika mazingira yote ya kazi kama *client.* Hii inaweza kuwa katika idara yeyote hata mahali kama hospitali siku hizi wanamwona mgonjwa ni *client* siyo tu wa kuonewa huruma na kwa sababu daima mteja ni mfalme na mtu yeyote anayehudumia akitambua kuwa mteja ni mfalme, basi ataweka nguvu zake zote na jitihada zote ili asimpoteze yule mteja. Lakini ukianza kusema tu kwamba mimi niko kwenye nafasi, mimi ndiye ninayeshika faili basi huwezi kumhudumia na ndiyo maana tunapata lugha chafu, ndiyo maana watu hawana haraka katika kutoa huduma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika hotuba ya upinzani katika ripoti zetu nyingi ukitafuta *result oriented* una maanisha kwamba lazima kufanya *appraisal* ya namna fulani au tathimini ya aina fulani. Lakini kwa uzoefu wetu tathmini hizi zinaweza zikaandikwa tu mezani na kama zinaandikwa mezani hutapata ubora unaohitaji. Kwa hiyo, nadhani umepata *result* lakini ulichopata ni taarifa iliyoandikwa tu mezani lakini ukisema ni *customer oriented* lazima katika *assessment* yako utafanya vilevile kama ile *assessment* inamgusa namna gani yule *client* yaani yule anayehudumiwa. Kwa hiyo sisi tunasema kwamba katika sheria yetu ni vema tukaiweka hii dhana ya result *oriented* iwe ni *result oriented* na *customer oriented* iwe na dhana zote mbili kwa pamoja kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme vilevile kwamba dhana hiyo inaungana na *perfomance assessment* zinazofanyika. Ni kweli kwamba *perfomance* ya wafanyakazi wetu au watumishi wetu wa umma tunaweza tukazifanya kwa kutumia *tools* au *instruments* tulizozi-*design*, *forms* na kadhalika na *perfomance* hizi tunafanya tathmini kama tulivyokwisha kuziangalia huko nyuma lakini hofu yetu ni kwamba mara nyingi unapofanya *perfomance* ya mtu, *perfomance* haiangalii tu kile mlichokubaliana kwamba atatekeleza kazi hizi ndani ya muda huu, mtumishi anayepaswa kuangalia au kusimamia kilimo, anayepaswa kuangalia mifugo, anayefanya kazi hospitalini atafika labda ofisini saa fulani , atahudumia labda watumishi kadhaa, atakwenda kutembelea mashamba kadhaa. Sasa hilo peke yake haiwezi kutosha na tutakuwa hatuwatendei haki watumishi wetu kama sisi tutaweka sheria lakini hatuwapi kwa upande wa pili nyenzo zinazotakiwa. Nadhani ni vema katika kuweka hizi *instrument* ili sheria zetu zipate maana, ili sheria zetu zisiwe za kuwekwa tu kwenye makabati, ni vema kabisa tunapoweka hii hatua ya pili itakayofuata ni kuangalia ni namna gani sheria hii itatekelezwa. Ni kukubaliana sisi kama Wabunge tunatunga hiki kifungu tunakiingiza kwenye sheria lakini baadaye tusipoangalia pia kwa upande wa pili tunakwenda kuwapima lakini hatujawapa nyenzo tunakuwa hatuwatendei haki watumishi hao. Mfano unaotolewa ni sahihi na mimi naurudia kusema hivyohivyo. Huwezi kutegemea Bwana Shamba ambaye anatembelea Kata nzima hana hata baiskeli ukategemea unaenda kumfanyia *perfomance assessiment* kwa sababu tu ya kutembelea yale mashamba. Huwezi kutegemea Bwana Mifugo akatembelea mifungo, akaenda kutibu ng’ombe wanaoumwa wakati hujampa hata baiskeli, hujampa hata dawa vilevile wakati huohuo hazipo dawa za kwenda kutibia wale mifugo hawa watu wanapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kupata mfano mmoja katika zahanati yangu. Nilimkuta Nesi ameacha kituo chake na kwanza kwenye eneo hilo Nesi yupo peke yake ameondoka amerudi nyumbani kwake wakati wa kazi. Mimi nikapata uchungu sana kwa sababu yule mama aliyemlita mtoto, mtoto karibu anapoteza fahamu nikapaswa kumfuata nesi nyumbani kwake. Nilipofika nyumbani kwa Nesi nilimkuta amekaa ndani wala hafanyi kazi amejikalia tu. Nikamwuuliza mama vipi akaniambia Dr. hata mimi ni mwanamke usifikiri nitakuwa tayari nimwone mtoto anakufa mbele yangu kwa sababu sina hata Asprin.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unapofikiria kwamba unaenda kupima *perfomance* ya mtu huyu unapima vipi? Hayuko kwenye kituo, hayuko kazini kwa wakati

anapotakiwa kuwa kazini lakini kwa nini hayupo kazini? Mimi niliumia kwa sababu aliniambia mimi ni mwanamke ninajua uchungu wa kumpoteza mtoto, nisingeweza kuvumilia namwangalie mtoto huyu anakufa mikononi mwangu kwa sababu sina hata *Asprin* ya kumsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni suala la *perfomance,* unaipima vipi hapa? Kwa hiyo, nadhani ni suala la kutunga sheria. Ni vema tuangalie pia sheria tunayoitunga basi kwa upande wa pili sisi tusaidie kuwawezesha hawa tunaotaka kuwapima kwa kuwapatia nyenzo, vifaa vyote vile vinavyotakiwa katika kutekeleza wajibu wao, ili tunapowapima tuweze kuwapima kweli kwa haki na waweze wao sasa kusema mimi nimewajibika hata ninapochukuliwa hatua ninachukuliwa hatua kwa sababu sikutekeleza kweli wajibu wangu lakini vinginevyo tutakuwa hatujatekeleza kweli wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo sana hili suala la ajira na kwamba nafasi zinapotokea waweze kuchaguliwa kwanza wale walioko kwenye idara husika, kama ni kwa kuangalia *seniority* basi nafasi zile zijazwe na yule aliyekwisha kuwepo au wale walioko kule wapewe haki ya kuomba sawa na wenzao. Mimi sina tatizo na utaratibu huo nadhani katika utawala na katika utawala wa usimamiaji wa watumishi, moja ya njia ya kupata na kujaza nafasi ni katika kuwapandisha wale waliopo kwenye idara hiyo, lakini wenzetu wanatumia utaratibu huo kwa kuuongezea na kuwekea vigezo. Kwa mfano mtumishi anatakiwa awe anajiendeleza kila wakati kwa hiyo unapopandishwa kutoka kwenye nafasi ulioko kwenda kwenye nafasi ya juu zaidi unatakiwa uwe umepata sifa inayotakiwa katika kitengo hicho si kwa sababu tu ulikuwa ndani ya Idara kwa hiyo sasa unapanda *automatically* kwa sababu wewe ndiyo *senior*. Mimi nadhani tutakuwa tunakosea sana kama tunakwenda kwa utaratibu huo bila kuangalia kwamba wanaopandishwa nao wana sifa za kiwango gani., katika hali tuliyonayo sasa na tunakokwenda huko mbele kila mwaka tunapata vijana wapya wanaomaliza vyuo vikuu, kwa hiyo tuna watu wenye sifa kwa kila eneo. Ni kweli anayepata cheti leo inawezekana uzoefu wake si mkubwa na hata kazi hawezi kuitekeleza sawa na yule aliyekuwepo, lakini kwa maana ya sifa basi ni vizuri tukaangalia kwamba kila mtu anaingia kwenye nafasi kutokana na sifa aliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya uzoefu unatuonesha na ukienda mitaani sasa hivi Watanzania wengi wanalalamika kwamba unapotafuta kazi, unapoomba hata kama ilitangazwa usipokuwa na *referee* huwezi kupata ajira. Mimi nadhani Waziri ana nafasi nzuri leo ya kulitangazia Taifa kwamba hiki kitu tulishapiga vita nadhani tumefanikiwa kuiondoa kwa kiwango kikubwa lakini tupate matumaini bado kwamba hakuna *referee* tena katika kutafuta ajira nchi hii. Suala la undugu, suala la kumfahamu fulani, suala la kwamba nina *God father*, haya ni masuala yanayodidimiza morali ya watumishi wetu. Nafasi za ajira zinatangazwa, watu wanaamini kabisa inapotangazwa ni kiini macho tu kwa sababu kuna watu waliokwisha kuandaliwa na kwa sababu kwenye bodi za ajira wanajua kuna fulani na fulani ana ndugu zake hawa na hawa basi mimi sitapata mpaka nitafute *referee* na ndiyo maana Wabunge tunapigiwa simu mara nyingi nadhani Wabunge wengi tu wanapata adha hiyo kwamba mzee kuna ajira imetangazwa naomba nisaidie. Sasa hii ni dhana ambayo inaendelea kudidimiza utumishi wa umma. Ni kweli kwamba kama tunahitaji kusaidia tusaidie tu kwa kuonesha, tuwaoneshe labda

wapiga kura wetu kwamba kuna nafasi mahali fulani. Lakini mimi huwa nikiombwa nisaidie pale huwa nakataa na ninatamka kabisa kwamba huwa nakataa kumsaidia mtu kuingia kwa sababu anayenifikia ni yule mwenye uwezo na yule asiye na uwezo lakini asiye na uwezo lakini anasifa na yeye anapataje ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukiweka msimamo wa namna hiyo tunaweza tukapata watumishi wazuri wa umma, tunaweza tukajenga morali kwa watumishi wetu na tunapozungumzia kwamba tunaimarisha sheria ili watumishi wetu wetu wapate pia namna nzuri ya kuhudumia watu wetu nadhani kunaweza kuwa na nguvu ya kutoa utumishi mzuri kwa sababu tumejenga misingi ya kupata ajira ambayo haitegemeani na ma-*referee* kwa kujuana na fulani na fulani au kwa kuwa na G*od father* mahali fulani. Napenda Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. Najua kwamba jitihada zinafanyika, najua kwamba kuunda Tume za Ajira zote hizi ni jitihada za kuondoa nani anamfahamu nani, lakini bado katika mawazo ya Watanzania haijaondoka kwamba bila *referee* huwezi kupata ajira sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimalizie tu kwa kusema kwamba sheria hii itatusaidia lakini sehemu iliyozungumzwa na msemaji wa upinzani ya kuweka wazi mgawanyo kati ya mamlaka za Halmashauri ziwe za miji, ziwe za jiji, ziwe za Wilaya na mamlaka hizi zingine za Serikali kuu bila kutenganisha hii nadhani tutakuwa tunafanya makosa makubwa.Kwanza mamlaka ya Serikali za Mitaa inaongozwa kwa sheria zake maalumu, kuna waamuzi ambao wamewekwa mahususi na sheria na hawa ni Baraza la Madiwani lakini ni nani hasa anayefanya uamuzi, je mwajiri pale katika Halmashauri ni Mkurugenzi au ni wale Madiwani, wenye kufanya uamuzi wa mwisho ni Madiwani au ni Mkurugenzi yule anayesimamia Halmashauri kwa niaba ya Madiwani? Sasa tusipoweka hii mara nyingi tunapata malalamiko na Waheshimiwa Wabunge kama huwa wanafuatilia kwa karibu nadhani mnaona mgogoro wa namna hii. Mkurugenzi analeta kwenye Baraza la Madiwani lakini na yeye atakuwa amefanya maamuzi yake. Madiwani hata wakitaka kushauri anasema mimi ndiye mwenye mamlaka ya nidhamu, mimi ndiye mwenye mamlaka ya ajira, sasa tusipotenganisha haya nadhani tutaendelea kupata mgongano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tunajadili Sheria Na.8 tulisema tuweke wazi tofauti hizi lakini mpaka leo nadhani hatukufikia kiwango tunachotaka. Najua kwamba ilijaribiwa kurekebishwa lakini hatukufikia kiwango tulichokuwa tunakisema wakati tukijadili Sheria Na. 8. Kwa hiyo, ningependa hii ya leo liweze kuwekwa wazi ili tuepuke mamlaka kati ya mamlaka zetu za kisheria kwa maana ya sheria zinazosimamia mamlaka za Jiji, Halmashauri za Wilaya na za Manispaa na mamlaka za Halmashauri Kuu ambazo ziko wazi zaidi kutokana na sheria yake kuwa wazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemalizia kwa kusema kwamba utumishi wa umma unafanana, iwe katika Serikali Kuu au iwe katika Serikali za Mitaa na iwe *Executive Agency* za Serikali, hawa wote ni watumishi wanahudumia wananchi na *at the end of the day* anayehudumiwa ni mwananchi yule yule iwe anahudumiwa na Serikali Kuu iwe anahudumiwa na Serikali za Mitaa, iwe ni *Agency* hatimaye anayehudumiwa ni mtu yule

yule. Kwa hiyo ni vema ukaweka wazi mipaka ya kila mmoja katika maeneo haya. Hata *Executive Agencies* nazo zinatakiwa zikawekewa taratibu zake zilizowazi zaidi kufuatana na sheria ya *Executive Agencies* ambayo tulipitisha ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba nashukuru na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu kwa wakati huu ili tuweze kuimarisha utumishi wa umma. Pia ningependa nimalizie zaidi kwa kusema kwamba ile *client charter* tuliyoisema tunaomba basi ukaifanyie kazi vizuri isiwe imebaki na yenyewe katika vitabu kwa sababu wananchi bado wanalalamika. Kwenye matangazo bado tunaona yale yaliyoahidiwa kwamba barua zitajibiwa, watu watahudumiwa kwa haraka, hayajaonekana na leo tunakuja na marekebisho mengine ambayo tunataka yafanye kazi lakini tusije tukaangukia katika mtego ule ule.

Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kama nilivyosema mimi sina orodha nyingine ya wachangiaji kwa hiyo nitamwomba Mheshiwa Waziri wa Nchi, Utumishi ajaribu kujibu au kufafanua yale yaliyozungumzwa.

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kutuwezesha kuwasilisha Muswada wetu na wachangiaji kujitokeza japo ni mmoja, lakini pia napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wazungumzaji wote waliochangia Muswada huu.

Kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Utawala Bora. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Grace Kiwelu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora na mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kuchangia katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa. Kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alisema alikuwa anapendekeza Waheshimiwa Mawaziri na wenyewe wapewe uwezo wa kuweza kuchagua Wenyeviti wa Bodi. Ningependa kumhakikishia kwamba sasa hivi tuko katika mchakato jinsi gani tunaweza tukapunguza baadhi ya mambo kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu ni kazi ngumu kwake na ana majukumu mengi. Lakini kwa asili ya Ofisi yangu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mkuu wa Utumishi wa Umma ni Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, suala la kuchagua Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Ajira bado linabaki kwake kwa kuwa yeye ndiyo Mkuu wa Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu sasa hoja zilizotolewa haswa na Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo. Mheshimiwa Grace Kiwelu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema kwamba katika mapendekezo yetu tumezungumzia sana *result oriented management* na kwamba peke yake haiwezi kutosha bila kuwa na *customer oriented.* Napenda kutoa ufafanuzi kwake kama ifuatavyo. Hiyo *customer oriented* anayoisema hiyo ni kama *tool* ambayo inaweza kutufikisha kuwa na *result oriented* na katika Ofisi zetu za Serikali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na katika Halmashauri zetu za Serikali za Mitaa, suala la kumjali mteja limewekwa mbele kama njia mojawapo ya kuufanya utumishi wa umma ufanye kazi kwa ufanisi na Wizara zote zinatakiwa ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi ili tuweze kupata matokeo katika utumishi wa umma, ni lazima kila Wizara iwe na mpango mkakati ambao ndani yake unazingatia matakwa ya mteja. Lakini pia ni lazima kila Wizara iwe na mkataba wa huduma kwa mteja. Ili kuwa na ufanisi na katika ziara zangu nyingi ambazo nimepita Mikoani na hata katika kipindi chetu cha maboresho ya utumishi wa umma kwa wale ambao wanafuatilia suala la mkataba wa huduma kwa mteja tumelipa kipaumbele sana na katika ule mkataba wa huduma kwa mteja, tumezitaka taasisi za Serikali zote ziainishe huduma wanazozitoa kwa wananchi na pia ionyeshe kwa kiwango gani na kwa muda gani na pia tumewataka wananchi kama wateja na wenyewe walalamike pale ambapo wanaona zile huduma hazitolewi kwa viwango na kwa muda ambao umeainishwa katika ile miakataba ya huduma kwa mteja. Kwa hiyo bado ninarudia kuwaomba wananchi na sisi tukiwa Wabunge bado tulalamike pale ambapo tunaona huduma haziendi kama vile tulivyokusudia na pale tunapoona kwamba watumishi wetu wa umma wanatoa huduma sivyo ambavyo Serikali inataka ili tuweze kuwarekebisha na tuweze kurekebisha na ufanisi ule tunaouzungumzia uweze kufikiwa. Lakini pia ili mtumishi mmoja mmoja aweze kufanya kazi kwa kumjali mteja na ili aweze kuleta ufanisi uliokusudiwa na Serikali ndipo pale ambapo tunampima utendaji kazi wake na tunaingia naye mkataba yeye binafsi na huo ndiyo tunaufanya mkataba kwa uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ule upimaji wa utendaji kazi wa mtumishi tunaingia mkataba baina ya mtumishi na yule mwajiri wake. Katika ule mkataba wa huduma kwa mteja ni mkataba baina ya taasisi ile na wananchi. Sasa ili taasisi iweze kufanya kazi vizuri ndiyo tunaingia sasa mkataba wa mtumishi mmoja mmoja na mwajiri wake. Sasa katika ule mkataba ni lazima ataainisha ni kazi zipi atazifanya ndani ya mwaka mmoja au ndani ya miezi sita na ili aweze kufanikisha yale ambayo ameyakusudia kuyatekeleza itabidi aainishe rasilimali ambazo atahitaji ili aweze kufikia ufanisi na pia tunakuwa na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Wilbrod Slaa kwamba tunaposema *result* hatumaanishi taarifa ya mezani. Tunachotaka pale ni je huduma ya taasisi husika imefanyika? Kama ni kuwahudumia wagonjwa, wamehudumiwa kwa muda unaotakmiwa na kwa viwango vinavyotakiwa? Kwa hiyo hivyo vitu vyote tunaviunganisha kutokea tangu ule mkataba, mpango mkakati wa ile taasisi lakini pia mkataba wake na wateja na pia mkataba wa mwajiri na mtumishi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la kuwajengea uwezo na kuwapatia vitendea kazi. Kwa hiyo, kama nilivyosema, nilivyojibu pale mwanzo katika ule mkataba wa mtumishi mmoja mmoja yeye na mwajiri wake ndipo pale ambapo yeye atasema ili aweze kufanya kazi vizuri anahitaji kujengewa uwezo wa aina gani na anahitaji nyenzo gani kutegemea na uwezo wa taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa ni suala ya Mamlaka ya Ajira katika Serikali za Mitaa. Napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Mamlaka ya Ajira katika Serikali za Mitaa ni Baraza la Halmashauri. Utendaji wa kazi katika Serikali za Mitaa ni tofauti na utendaji kazi katika Serikali Kuu. Utendaji kazi katika Serikali za Mitaa, unaendeshwa kwa vikao. Kwa hiyo, Mkurugenzi peke yake hawezi kuwa na mamlaka akasema kwamba mimi nimeamua hivi. Utendaji kazi au Mamlaka ya Ajira katika Serikali za Mitaa ni Mamlaka ya Serikali husika *Local Government Authority* ile ndiyo mamlaka ya ajira. Kwa hiyo, pale haiku-*specify* kama ilivyokuwa katika Utumishi wa Serikali Kuu kwamba ni Katibu Mkuu, kule tunasema ni *Local Authority*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la ujazaji wa nafasi kwa sababu suala la wale wanaoanza kazi, suala la usaili liko kama kawaida. Hapa tunazungumzia suala la upandishwaji wa vyeo na ujazaji wa nafasi hasa katika utumishi wa umma. Ndiyo maana hizi nafasi zinazojazwa au upandishwaji wa vyeo tunataka mtu ambaye ana uzoefu na utendaji mzuri. Sasa siyo rahisi kuweza kujua ufanisi wake na ubora wake kwa mtumishi ambaye yuko nje ya utumishi umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatekeleza Sheria Na. 8 ya mwaka 2002, tuliacha wazi kwamba tunaweza kujaza vyeo, nafasi hizi za uandamizi kwa kutangaza. Lakini uzoefu tulioupata mara nyingi tuliowachukua kutoka nje ya utumishi wa umma wamechukua muda mrefu sana kujifunza kuielewa Serikali inafanyaje au utumishi wa umma unafanyaje kazi. Sasa kutokana na upungufu huo, tumeona ni vizuri ili suala la kumtafuta mtu kutoka nje ya utumishi wa umma iwe ni chaguo la mwisho baada ya kuwa ndani ya utumishi wa umma tumekosa kabisa mtu mwenye sifa, mwenye uwezo ndipo hapo tutangaza na kuhitaji mtu kutoka nje ya utumishi wa umma. Kwa lile suala la kusema kwamba hatutendi haki, kwa kweli haki inafanyika na tunaf anya hivyo kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, s*eniority list* itaangaliwa, lakini yule aliyeko pale ambaye tunamwona ni *senior* tukiona uwezo wake ni mdogo pamoja na kwamba unaweza kuwa na *qualification* tutajaribu kuangalia kutoka katika Wizara nyingine ndani ya utumishi wa umma. Tukiona pia hata katika Wizara nyingine ndani ya utumishi wa umma, hakuna mtu mwenye uwezo, mwenye sifa tunazozihitaji, hapo tutatangaza kutoka nje ya utumishi wa umma. Lakini siyo kipaumbele chetu kwamba turuhusu kila mtu kutoka nje ya utumishi wa umma kwa nafasi zile ambazo ni za Uandamizi.

Mhehsimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumziwa ni kwamba niwahakikishie Watanzania na nimhakikishie Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba kwa kiasi gani ubaguzi, upendeleo na suala la *referee* litaondoka katika utumishi wa

umma? Tunazo Sheria, tunazo Mamlaka zetu za Ajira na sasa hivi tunakusudia kuanzisha chombo ambacho kitasimamia, kitaanzisha huo mchakato wa ajira katika utumishi wa umma na kwa kweli tunataka kila mtu awe msimamizi katika suala hili ili kuhakikisha kwamba suala la ubaguzi, la upendeleo katika utumishi wa umma halipo. Lakini pia ili kuhakikisha kwamba upendeleo na ubaguzi katika ajira na upandishwaji vyeo halipo katika utumishi wa umma ndiyo maana tukawa na Tume ya Utumishi wa Umma na ndiyo maana hata leo tumeiomba katika marekebisho yetu iendelee kuwa Tume Rekebu na siyo Tume Tendaji. Yenyewe iwe msimamizi wa kufuatilia mamlaka zote za ajira na ndiyo kazi ambayo inaifanya, kuhakikisha kwamba inatenda haki, Mamlaka za Ajira zinatenda haki na kwamba hakuna upendeleo wala ubaguzi katika ajira na upandishwaji wa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama itaonekana kwamba baadhi ya maeneo ubaguzi umetendeka katika ajira au upandishwaji wa vyeo wanaweza kukata rufaa katika Tume ya Utumishi wa Umma na bado yenyewe huwa inafuatilia katika mamlaka mbalimbali za ajira kuhakikisha kwamba ajira na upandishwaji wa vyeo unafanyika bila upendeleo na ina mamlaka ya kumuita, kuita mamlaka yoyote ya Ajira, Mtendaji Mkuu yoyote wa mamlaka ya ajira na ikamuhoji na ina uwezo wa kufuta baadhi ya ajira kama itaonekana kwamba haki haikutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kwa kweli tunajitahidi kwa nguvu zetu zote kuhakikisha kwamba haki inatendeka na pia tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wanapoona kwamba kuna namna yoyote ya ubaguzi na upendeleo unatokea basi watupatie taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamliwa na Kuafikiwa)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007 *(The Public Service (Amendment) Bill, 2007***

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3(a)(i), pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilitaka Mheshimiwa Waziri anisaidie au anifafanulie. Inaelekea tunapozungumzia *results oriented* na sisi tukapendekeza

*customer oriented* ni kama tunazungumzia mambo mawili tofauti. Ukitazama sana *result oriented* inakazia suala la *quantitative* suala la *customer oriented* inachukua *dymension* ya *quality at assessment.* Sasa kwa *result oriented* mmekubaliana labda huyu mtaalam atahudumia heka 20 kule kijijini lakini *quantitative at assessment* inataka kuona ameihudumia vipi, kwa maana ya kwamba katika kumwa-*assess* yule mtaalaam wetu tutataka kujua na *atitute* anapomhudumia kwa sababu kuna tatizo sasa mtaalam anaenda kwenye eneo akafika pale akachungulia akachunguza akarudi akasema nimeona heka kadhaa zipo. Kwa kweli kwa maana ya *quantitative assessment* yake heka 20 zipo lakini *quality assessment* ambayo ndiyo lengo la Taifa kwamba tunataka huduma bora, yule mwananchi na yeye analalamika kwamba huyu hajanihudumia vizuri. Sasa tunapataje ile *assessment* ili tunapotengeneza sasa huu mkataba usiishie tu kwenye kupata takwimu ya idadi mliyokubaliana lakini tukakosa ule upande wa pili wa *quality?* Nilitaka Mheshimiwa Waziri anihakikishie hilo tunalipataje?

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Wilbrod Slaa kama nilivyotangulia kusema *result oriented* tunataka utumishi wenye matokeo. Hii ilitokana na kwamba mwanzo katika utumishi wa umma tulikuwa tunawapima watumishi wetu kwa kuangalia ameingia kazini saa ngapi, anaondoka saa ngapi lakini bila kujali mwisho wa siku anapoondoka amefanya nini ambacho tunaweza tukakiona. Sasa katika kuondoka na hilo sasa tukasema lazima twende zaidi kwenye mambo ya *result oriented.* Lakini anafikaje huko katika kuonyesha yale matokeo? Ndiyo maana nikasema kwamba kuna vitu ambavyo vinamfikisha huko kwenye *result.* Kwanza, ni lazima kuwe na mpango mkakati kwa kila taasisi ambayo utaonyesha ndani ya miaka mitano, kitu gani hiyo taasisi inatakiwa itoe na katika ule mpango mkakati ndipo sasa kitu kingine ambacho kinatakiwa tena kuna huo mkataba wa huduma kwa mteja ambao ni yeye anazungumza. Mimi nasema hiyo tunayo lakini ni kama *tool* tunayoifikia katika *result oriented*. Kwa hiyo, mimi sioni kama kuna utata wowote.

**MWENYEKITI:** Ukweli ni kwamba inategemea unataka kuangalia wapi, unaweza kuangalia *result oriented* ambayo *evaluation* yake lazima iwe *customer benefits* ambazo mnazo. Kwa kweli ni *symantics* tu, ni sawa. *Result* inatoka na kilichotakiwa kufanyika kimefanyika, mimi nadhani iko sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007 *(The Public Service (Amendment) Bill, 2007***

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Public Service Amendment Bill, 2007* pamoja na marekebisho yake kifungu hadi kifungu na kuukubali. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma *The Public Service Amendment Act, 2007* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

**Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa**

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment (No. 2) Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Mkutano huu wa Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mambo mengi yametokea tangu tuachane hapa mwezi Agosti, 2007 yapo mazuri ya kufurahisha lakini pia yapo ya huzuni. Hivyo naomba kuwapa pole ndugu na familia za wote ambao wamefikwa na mambo ya huzuni na hasa familia ya ndugu yetu Mheshimiwa Salome Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja ya kwamba Muswada wa Sheria uitwao *The Written Laws (Miscellaneous Amendment Bill (No. 2)* ya mwaka 2007 pamoja na mabadiliko yaliyoambatishwa katika Jedwali la orodha ya mabadiliko sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa kupitia na kuchambua Muswada huu na kwa ushauri mzuri ilioutoa kuhusu namna ya kuboresha maeneo mbalimbali ya Muswada huu. Ushauri huo umetusaidia sana katika kuuboresha na hivyo kuwezesha uwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii. Tunamshukuru kila Mjumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri aliyoifanya na kwa ushirikiano mzuri aliotupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unatoa mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho sheria tatu. Sheria hizo ni Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85, Sheria ya Silaha na Risasi za Moto, Sura ya 223 na Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya kwanza inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni sheria ya Alama za Biashara *(The Mechandize Marks Act, Chapter 85).* Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika maeneo kadhaa ili kuondoa kasoro zilizojitokeza katika utekelezaji wa masharti yake. Mapendekezo ya marekebisho yana lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanayopendekezwa kufanywa katika fungu la pili yanalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria kwa kumteua Mkaguzi Mkuu yaani *Chief Inspector* na kumpa mamlaka ya kusimamia, kuratibu na kutoa maamuzi katika masuala yote yanayohusu alama za biashara. Awali sheria hiyo ilikuwa inampa mamlaka Waziri anayehusika na masuala ya biashara kuteua Wakaguzi lakini hakukuwa na Mkaguzi Mkuu na hivyo kulikuwa na ugumu katika uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkaguzi ambaye atateuliwa na Waziri wa Biashara pamoja na mambo mengine atawajibika kuchunguza au kuamuru uchunguzi ufanyike kwa mtu yeyote ambaye atahisiwa kuvunja masharti ya sheria hii. Vile vile Mkaguzi Mkuu atakuwa na wajibu wa kufungua mashtaka Mahakamani dhidi ya wanaokiuka masharti ya sheria hii. Marekebisho haya yanalenga pia kumpa Mkaguzi Mkuu mamlaka ya kusikiliza malalamiko yanayoletwa kuhusu bidhaa bandia au zilizogushiwa na kuyatolea maamuzi kwa kufuata utaratibu ambao utawekwa na kanuni chini ya sheria hii. Sheria hii imezingatia umuhimu wa mtu kusikilizwa kwa ukamilifu na imewekewa

kifungu kinachoruhusu mtu kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mkaguzi Mkuu kwenda Baraza la Ushindani Sawa wa Biashara yaani *Fair Competition Tribunal.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii vile vile inamwekea kinga ya mashtaka au madai Mkaguzi Mkuu au mtu yeyote atakayetekeleza majukumu ya Mkaguzi Mkuu kwa yale atakayofanya wakati akitekeleza chini ya sheria. Rekibisho hili lina lengo la kuwafanya wahusika watekeleze wajibu wao bila woga lakini kwa nia njema ya kuhakikisha kuwa alama za biashara zinazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine linalopendekezwa kufanyiwa marekebisho linahusu Kanuni za utekelezaji wa masharti ya sheria. Fungu jipya la 18A linapendekezwa kuongezwa. Fungu hili linalenga kumpatia Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara uwezo wa kutengeneza kanuni ambazo zitaboresha utekelezaji wa sheria hii. Waziri kwa mujibu wa marekebisho anaweza kutengeneza kanuni zitakazoelezea utaratibu wa jinsi Mkaguzi Mkuu atakavyoweza kushughulikia na kuamua mashauri yanayowasilishwa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri pia anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kukamata, kuhifadhi na kuachilia bidhaa. Vile vile anaweza kuweka kanuni ya jinsi ya kukasimu mamlaka yake chini ya sheria hii. Kanuni hii itakuwa na fomu ambazo zitatumika chini ya sheria na zitaweka gharama, faini, adhabu ambazo Mkaguzi Mkuu anaweza kutoa katika mashauri yatakayowasilishwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya pili inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Silaha za Risasi za Moto, Sura ya 223 . Madhumuni ya marekebisho haya katika sheria hii ni kuoanisha aina ya adhabu zinazotolewa kwa kosa la umiliki wa silaha usio halali. Fungu la adhabu lililokuwepo lilikuwa linatoa adhabu ya kosa kama hilo chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya tatu inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuipatia Mahakama fursa ya kutoa adhabu inayozingatia kinga kwa watoto dhidi ya adhabu za kutweza na kuitisha majalada ya kesi ili kujiridhisha kwamba haki za mtoto haziendelei kukiukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 ilifanyia marekebisho Sheria ya Kanuni za Adhabu, mafungu 131 na 131(A) ya Sheria hiyo ambayo yanaitaka Mahakama kutoa adhabu ya kifungo cha muda mrefu kwa mtu yoyote anayepatikana na hatia bila kuzingatia umri. Marekebisho yanayopendekezwa yatawezesha Mahakama kutoa adhabu ya viboko kwa watoto watakaopatikana na makosa

ya kubaka chini ya sheria na vile vile kumpa uwezo Hakimu kutoa adhabu tahfifu kwa kuzingatia ushiriki wa kila mtoto katika kushiriki tendo la ubakaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza azma ya kulinda haki za mtoto, inapendekezwa liongezwe fungu jipya 160(B) ili kuruhusu Mahakama Kuu kurejea na kufanyia masahihisho adhabu zozote za kikatili zitakazotolewa na Mahakama za chini dhidi ya watoto hata kama zipo sheria zinazozuia marejeo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho katika sheria hii, yana lengo ya kuhakikisha kuwa haki za msingi za mtoto zinalindwa na kwamba adhabu ya kifungo kwa mtoto haitolewi kiholela kwani watoto wanatakiwa kurejeshwa katika maadili kwa adhabu ndogo na siyo kuwatenga na jamii kwa muda mrefu na hivyo kuwaharibia kabisa maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii na kupitia kwako kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Msemaji wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu, Mheshimiwa Pindi Chana kwa niaba ya Mwenyekiti *(Makofi)*.

**MHE. PINDI H. CHANA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2007 *(*The *Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa, natumia fursa hii kutoa salamu za rambi rambi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu na jamaa, kutokana na kifo cha ghafla cha Marehemu Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (CCM) na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, aliyefariki kwa ajali ya gari tarehe 24 Oktoba, 2007 katika kijiji cha Kibena, Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Iringa.

Vile vile natoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na familia za marehemu wote waliofariki katika ajali hiyo. Vifo vya marehemu hao siyo tu vimeacha pengo kubwa kwa familia zao, bali pia vimelipotezea Taifa watu muhimu ambao bado lilikuwa linawahitaji. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amen!*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu iliujadili Muswada huu katika kikao kilichofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar-es-Salaam, tarehe 16 Oktoba, 2007. Katika

kikao hicho Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Johnson Mwanyika, (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Kamati ilipokea maoni ya wadau kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(Legal and Human Rights Centre)*, yaliyowasilishwa na Bwana Leonard Elias na Bwana Doto Justo wa Shirika la Msaada wa Sheria (*National Organisation for Legal Assistance).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Mtoa Hoja, Muswada huu unazifanyia marekebisho sheria zifuatazo: Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85 (*the Merchandise Act, Cap 85),* Sheria ya Silaha na Risasi za Moto, Sura ya 405 (*Arms and Ammunition Act*, *Cap 405)* na Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 (*Penal Code, Cap 16).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati yetu ilikubaliana na Muswada huu, kwanza, kwa kuzingatia kuwa mapendekezo yaliyokusudiwa katika sheria zilizotajwa yana lengo la kuziboresha sheria hizo ili ziendane na wakati. Pili, kwa kuzingatia kuwa ushauri tulioutoa katika kikao cha Kamati ulikubaliwa na Serikali na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuujadili Muswada huu, Kamati yetu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa na kuhitaji ufafanuzi katika maeneo machache ambayo hayakueleweka vema. Serikali iliyafanyia kazi maoni yetu na kuupokea ushauri wa Kamati kwa lengo la kuuboresha Muswada huu. Kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, ushauri mmojawapo uliotolewa na Kamati unahusu Ibara ya 2D ya Muswada inayompa Waziri mwenye dhamana ya Sheria ya Alama za Bidhaa, mamlaka ya kukasimu madaraka ya Mkaguzi Mkuu (*Chief Inspector)* wa alama za bidhaa kwa watu wengine au vyombo ambavyo Waziri anaweza kuelekeza au kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitafakari kwa kina neno kushauri (*advise)* kama lilivyotumika katika Ibara hii na kuona kwamba kimsingi jukumu la ushauri ni la watendaji na Waziri kazi yake ni kuelekeza. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilishauri kuwa neno *advise* lisitumike katika Ibara hii na badala yake sentensi ioneshe Mamlaka ya Waziri kutoa maelekezo kama ifuatavyo: *The Powers of the Chief Inspector may be delegated to such persons or public institutions as the Minister may direct.* Napenda kutoa taarifa kuwa ushauri huu ulipokelewa, na Serikali iliahidi kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilitafakari kwa undani pendekezo lililopo katika Ibara ya 2B (1)(C) inayompa madaraka Mkaguzi Mkuu kumkagua mtu yeyote ama akiwa peke yake au mbele ya mtu mwingine, kwa kadiri atakavyoona inafaa kulingana na mazingira ya masuala yanayohusiana na sheria hii.

Kamati iliona kuwa kwa hulka za kibinadamu madaraka ya namna hii yakitekelezwa na Mkaguzi Mkuu peke yake inawezekana yakatumika vibaya. Kwa sababu hii, Kamati ilishauri kuwa Serikali ingeangalia uwezekano wa kumwongezea wakaguzi wengine. Hata hivyo, Serikali iliihakikishia Kamati kuwa mkaguzi atakayeteuliwa atakuwa ni mwadilifu na kwamba hata akiwa peke yake atatekeleza wajibu wake ipasavyo. Pamoja na hayo Kamati inashauri kuwa Serikali iwe makini

katika kufanya uteuzi huo na kufuatilia kwa karibu utendaji kazi wa Mkaguzi Mkuu hasa ikizingatiwa kuwa si rahisi kupima uadilifu wa mtu kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya V ya Muswada inayofanya marekebisho katika sheria ya Kanuni za Adhabu *(Penal Code, Cap 16),* Kamati iliafikiana na maelezo ya Serikali kuwa marekebisho yaliyokusudiwa yana lengo la kuwalinda watoto dhidi ya ubakaji.

Pamoja na hayo, Kamati ilishauri kuwa kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji kuna umuhimu mkubwa wa kutazama upya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana na adhabu zinazotolewa kwani baadhi ya adhabu hazioneshi kama zinasaidia kuwarekebisha wahalifu. Kwa kuwa Serikali ilitoa taarifa kuwa suala hili limepelekwa kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria na linafanyiwa kazi, Kamati inasisitiza kuwa Tume hiyo ijitahidi kuzungumza na wadau mbalimbali na marekebisho ya sheria hiyo yaangalie jinsi sheria itakavyowadhibiti kikamilifu watu wenye tabia ya kuwabaka watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yalihusu ufafanuzi ambao kwa kiasi kikubwa Serikali imetoa melezo ya kutosha na kuiridhisha Kamati. Mwisho, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia namshukuru Mheshimiwa Johnson Mwanyika, (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wake kwa kuwasilisha vema Muswada huu kwenye Kamati. Vilevile nawashukuru wadau kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(Legal and Human Rights Centre)* na Shirika la Msaada wa Sheria *(National Organisation for Legal Assistance),* kwa maoni yao yaliyoisaidia Kamati.

Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa michango yao ya kina iliyouboresha Muswada huu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo: Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Shoka Kh. Juma, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Abas Z. Mtemvu Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Halima Mdee, na mimi Mheshimiwa Pindi Chana. *(Makofi).*

Vile vile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Emanuel Mpanda, kwa kuhudumia vema Kamati wakati wote wa kuuchambua Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu, na naomba kuwasilisha *(Makofi).*

**MHE. NAIBU SPIKA:** Asante, sasa nitamwita msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Maghimbi. Kuna wasemaji wawili tu nafasi ipo. *(Makofi)*

**MHE. FATUMA M. MAGHIMBI (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kan. Na. 45(3) (b) na (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Salome Mbatia. Pia natoa pole kwa jamii nzima ya Wanawake wa Tanzania bila kujali itikadi zao kwa kumpoteza kiongozi huyo mwenye mwamko wa kupigania haki za sisi Wanawake na kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amen!*

Naomba pia kutoa pole kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Upinzani, kwa kufiwa na mama yake mpendwa wakati hili linapotokea na yeye mwenyewe yuko kwenye matibabu nje ya nchi. Pia pole kama hizo zimwendee Mheshimiwa Mustapha Mkulo, kwa kufiwa na mama yake mpendwa. Naomba nao Mwenyezi Mungu awape moyo wa ustahamilivu. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa wengine ambao nao wamekumbwa na masahibu mbalimbali, naomba Mwenyezi Mungu awape roho ya ustahamilivu na kusubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya rambi rambi zangu hizo, sasa naomba kutoa maoni juu ya marekebisho ya *Merchandise Marks Act* iliyotungwa 1963, na tangu mwaka huo sheria hiyo haifanyi kazi. Sasa wakati muafaka umefika kwa Sheria hii kubadilika na kufanya kazi. Katika ibara ya 6 ya muswada, Kifungu kipya cha 2B (1) (c) ambacho kinasema, naomba kunukuu, "*The Chief Inspector shall... have powers... to examine any person either alone or in presence of any other person.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba wakati wa kukagua awepo mtu mwingine. Sheria zetu za kufanya upekuzi *(search)* zinataka awepo mtu kama shahidi, kwa mfano, Mjumbe wa Nyumba Kumi, Katibu Kata au kiongozi mwingine yeyote, kuwapo kwa ushahidi ili wasiweze kumpandikizia vitu vibaya wakati wa kumkagua.

Kifungu cha (2) kinasema kama *supplier* hatatoa habari inayotakiwa basi atajulikana kuwa yeye ndiye *manufacturer*, yaani mtengenezaji. Kama huyu *supplier* anachukua bidhaa kwa tajiri ambaye siye *manufacturer* ataweza vipi kutoa habari ya *manufacturer* na wakati hajui *manufacturer* mwenyewe ni nani?

Kama anamjua *manufacturer* lakini *manufacturer* anakataa kutoa habari kumpa huyu *supplier* itakuwa sio haki kuchukulia kuwa *supplier* ndio *manufacturer*. Tume ya Ushindani ifanye juhudi kumpata *manufacturer* ili iweze kumwadhibu. Maana yeye ndiye mwenye makosa na Tume hiyo ndiyo yenye Mamlaka kisheria kuliko mnunuzi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine *supplier* anaagiza kwa mfano *TV* aina ya *Sony,* analetewa *TV* za Kichina lakini juu ya *TV* hizo imeandikwa *Sony,* je, yeye *supplier* anakosa gani katika mazingira haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie uwezekano wa Tume ya Ushindani kuorodhesha majina ya *manufacturers* wote ambao bidhaa zao zinatumika sana hapa nchini na kukagua viwanda vyao pamoja na bidhaa hizo mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa zina ubora unaotakiwa. Hili ni muhimu sana ikizingatiwa kuwa vifaa na bidhaa nyingi zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinatengenezwa katika mazingira mbalimbali kama vile *under license.* Bila kuweka utaratibu madhubuti na wa makusudi, mabadiliko haya ya Sheria hii nayo hayatafanya kazi kama ilivyoshindikana toka kutungwa mwaka 1963.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hiyo ambayo inasababisha maduka mengi ya wafanyabiashara kujaa bidhaa zisizokuwa na ubora (*fake material),* Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia kwenye Tume ya Ushindani, kuwafunza wananchi jinsi ya kutambua bidhaa za kughushi kwani wamepata hasara kubwa amabayo inaendelea kutokea hasa kwenye bidhaa za *electronics* na umeme bila kusahau bidhaa za vyakula ambazo zimewaletea matatizo baadhi ya watumiaji wa vyakula hivyo vinavyouzwa madukani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 6(b) ya muswada, kifungu kipya cha 2C(1) na (2), Kambi ya Upinzani tunapendekeza uwekwe utaratibu wa namna ya kuendesha kesi za rufaa. Tanzania tuna upungufu wa mahakimu, hivyo basi ni vyema kuweka utaratibu maalumu wa kusikiliza rufaa ili kesi ziweze kusikilizwa haraka kwa manufaa ya wafanyabiashara wasipoteze muda wao wa biashara kwani biashara yoyote inaenda na muda. Urasimu wa Mahakama unaweza si tu kuwagharimu wafanyabiashara peke yao bali pia uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 6(b) ya muswada, kifungu cha 2F(1), Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni bora kabla ya Mkaguzi Mkuu au mtu yeyote mwenye dhamana ya kufanya kazi ya ukaguzi, kabla hajaajiriwa ni bora atoe tamko la biashara zake alizonazo na aina ya biashara hizo. Jambo hili ni muhimu kuepuka kabisa uwezekano wa kuwepo na mgongano wa maslahi (*conflict of interest),* kwani si rahisi kwa mtu huyo akishakuwa na madaraka hayo kusema kwamba ana *pecuniary interest* katika suala analotakiwa kulifanyia kazi. Kwa kuzingatia ukweli kuwa katika jamii yetu maadili ya kiuendeshaji yanazidi kuporomoka kila kukicha, njia ya kurudisha maadili katika mstari ni Sheria kutamka bayana nini kinatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 6(c) ya Muswada, kifungu cha 18A(1), kifungu kidogo cha (2)(c), kinaweka utaratibu wa kukamata na utunzaji bidhaa zilizokamatwa. Kwa kuwa katika hatua hii kesi zimekwishamalizika na kuweka bidhaa katika sehemu salama kunahusisha gharama mbalimbali, ni vema Serikali itamke wazi ni nani anatakiwa kugharimia gharama hizo. Ni Serikali au yule mwenye hatia? Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaona kuwa inapothibitika kuwa na ukiukwaji wa taratibu zinazohusu Sheria hii ni bora bidhaa hizo ziharibiwe haraka ili kusiwepo nafasi ya

kufanya ujanja wa aina yoyote wa kuweza kuzirudisha kwenye masoko. Hili, vilevile litapunguza gharama kwa Serikali kuweka bidhaa hizo kwenye *safe custody*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya V ( *Part 5)* ya Muswada, ni marekebisho ya Sheria ya Kanuni za Adhabu. Katika ibara ya 10(a) ya Muswada inayofanya marekebisho katika kifungu cha 131cha Kanuni za Adhabu kwa kukifuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka kifungu kipya kinachosomeka, naomba ninukuu: "...*a person who commits an offence of rape of a girl under the age of ten years shall on conviction be sentenced to life imprisonment"*. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kosa hili isiwe kwa wale wanaofanya vitendo hivyo kwa watoto wa kike tu bali vilevile wale wanaofanya vitendo hivyo kwa kulawiti watoto wa kiume wadogo. Hivyo basi neno *girl* libadilishwe liwe *child*. Pia tunapendekeza wahusika wa kitendo hicho wahasiwe kabisa, kwani wanapoadhibiwa kifungo cha maisha wanaweza kupata msamaha wa Mheshimiwa Rais. Hivyo basi, ili kuwa na uhakika kama wakitolewa wasiweze tena kufanya kitendo hicho, wahasiwe. Najua wanaume wengi hawataipenda adhabu hii. Kambi ya Upinzani inatambua pia wapo wanawake wanaobaka watoto wa kiume kwa sababu yoyote ile kama ilivyojitokeza hivi karibuni katika jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa ubakaji unatokana hasa na ugonjwa uliomo ndani ya kichwa (*perversion)*, na hivyo unahitaji adhabu kali. Inahitajika adhabu kali inavyowezekana kwani kwa kifungo cha maisha ugonjwa huu unakuwa haujatibika, manake bado umo kichwani na hivyo pale ambapo mhalifu atakapopata msamaha kwa sababu yoyote ile ataweza kubaka tena anapofunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 10(b)(ii) ya Muswada inayofanya marekebisho katika kifungu cha 131A cha Kanuni ya Adhabu, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3), mbali ya adhabu iliyotajwa katika kifungu hicho kwa wanaohusika na ubakaji wa kikundi, ni bora wahusika hao wahasiwe ili wasifanye tena kitendo hicho katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kambi ya Upinzani haina matatizo yoyote ya marekebisho ya Sheria *the Arms and Ammunition Act.* Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha *(Makofi).*

**MHE. NAIBU SPIKA:** Asante! Mheshimiwa, naomba ukikaa pale tufanye marekebisho katika kifungu ulichonakili. Nenda kakae kwanza! Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alipotoa hotuba yake alisema anafanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 45(3)(b) na (c), Toleo la 2004.

Ukisoma Kanuni hiyo inazungumzia habari nyingine kabisa, wala haihusiani kabisa na kazi anayofanya. Kanuni ya 45(3) inasema, "hoja zifuatazo zaweza kutolewa bila taarifa," yaani: (b) hoja ya kuahirisha Bunge au kuahirisha mjadala; na (c) hoja ya kumsimamisha kazi Mbunge. Kwahiyo, nafikiri alitaka kutumia Kanuni ya 43(5) ambayo inasema: "endapo hoja haikupelekwa kwenye Kamati na imewekwa kwenye orodha ya shughuli au kama ilipelekwa kwenye Kamati na Kamati hiyo imemaliza

kuishughulikia na imewekwa kwenye orodha ya shughuli, hoja itawasilishwa na kuamuliwa Bungeni kwa kufuata masharti yafuatayo:-

(b) Mara baada ya Waziri au Mbunge mwingine anayehusika kuwasilisha hoja yake, Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa hoja hiyo atatoa maoni ya Kamati yake juu ya hoja hiyo; na

(c) Baada ya hapo kama hoja inayohusika ni hoja ya Serikali Msemaji wa Upinzania atapewa nafasi ya kutoa maoni ya upande wa Upinzani juu ya hoja hiyo.......” Kwa hiyo, nafikiri niiweke sawa ni Kanuni ya 43 (5) (b) na (c) na si kama mlivyosema. Nilisema kwamba tuna wasemaji wawili tu, kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii na mimi kutoa mkono wa pole na rambirambi kwa kufiliwa na kiongozi wetu mashuhuri, Naibu Waziri ambaye alikuwa ni mchapa kazi hodari katika Bunge ambaye alikuwa na uhusiano mzuri na kila kiongozi wa nchi hii. Pia na wengine wote ambao wamepata misukosuko ya aina mbalimbali. Mwenyezi Mungu *Inshallah* awape subira waliohusika nao pamoja na sisi. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu mwenyewe katika *Quran* kwamba *Innalillah wa Innalaih Rajuun*. Pili, nichukue nafasi hii kuchangia kidogo kuhusu hali ya biashara na marekebisho ya muswada huu ambao umeletwa mbele yetu leo.

Biashara inahitajia *capital* na kuna njia mbili au tatu ya kuweza kuipata *capital* kufanya biashara. Unaweza ukapata mkopo au ukapata *partner* akakupa *capital* wewe ukawa na *idea* ya biashara, ukafanya biashara ili uweze kuzalisha ukafaidika wewe na yeye. Lakini biashara ni *competition* vilevile na biashara ya leo *competition* yake imekuwa ni kubwa kwa sababu kuna nchi ambazo zimeinuka kibiashara na kuzalisha mali kwa wingi na ku-*supply* katika ulimwengu ambao bado haujazalisha mali hizo.

Sasa hii biashara imegawika katika makundi kama 5 ninavyoyaona mimi kwa hapa kwetu.Kuna biashara ya ku-*import* kutoka nchi za nje na kuna biashara ya ku-*export*. Ku-*export* bahati nzuri kunahodhiwa na Serikali yenyewe na mashirika makubwa na wafanyabiashara ambao wanasafirisha. Lakini kuna bishara ya kuleta ambayo imehodhiwa na watu wa kawaida, matajiri na watu wa kati. Sasa wanaleta bidhaa gani nchini? Huwa wanaleta madawa, chakula, vifaa vya *electronics, electrical spares* na viatu zaidi.

Lakini ukiangalia, tukianza na moja la madawa, kuna aina mbili, kuna madawa ya binadamu na kuna madawa ya wanyama, *thanks God*, madawa ya wanyama hasa hawa tunaowafuga huwa yanadhibitiwa vile vile na Serikali. Hatuna tatizo sana na baadhi ya dawa za binadamu ambazo huagizwa na Serikali kwa ajili ya hospitali zetu lakini kuna madawa ya binadamu ambayo yanaagiziwa na binadamu vilevile ambao hawana mkono na Serikali. Hapo ndipo kwenye hatari, madawa mengi yameenea hapa nchini ambayo utaona yameandikwa kwa lugha si ya Kiswahili tunachozungumza wala ya Kiingereza

kwa lugha yetu ya pili ambayo unaweza ukapata *prescription* kutoka kwa daktari au ukafahamu matumizi yake.

Sasa utaona dawa zile zimo mitaani na ni hatari kwa sababu unapotumia dawa kuna njia mbili, unaweza ukaifanya *body humanity* yake ikapotea kutokana na udhaifu wa dawa yenyewe uliyopewa au ukatumia dawa ikawa na *chemical* ambazo zikawa na madhara ya moja kwa moja katika kipindi kifupi. Mimi naona kwa hili suala la madawa Serikali idhibiti na iondoshe mara moja bidhaa zote ambazo hazina lugha mbili zinazoeleweka na kuweza kudhibitiwa na kitengo cha uagiziaji kutoka nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madawa hata ya meno utayakuta yameandikwa kwa lugha ya Kichina peke yake, kuna madawa ya ngozi, kuna madawa ya kunywa ya vidonge, yamo mitaani yanauzwa yameandikwa kwa lugha kama hii. Kwa hiyo, madawa yadhibitiwe ili tuondoshe athari inayoweza ikatokea mara moja kwa raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni kuhusu chakula. Kuna chakula cha nafaka cha makopo na maboksi kama *juice* na vitu vinginevyo tunavyovielewa na kuna mafuta ya kupikia. Haya vilevile yawe na viwango vya kuangaliwa uwezekano wa kwamba havitamwathiri binadamu. Leo Tanzania tuna matatizo mengi ya saratani *(cancer)* lakini hakujafanyika utafiti wa kutosha kujua hasa *cancer* inasababishwa na nini. Yawezekana huu uagizwaji wa kiholela wa kuwaruhusu wafanyabiashara kuingiza katika *super markets* bidhaa wakaziweka, muda wa matumizi yake ukatipata, hakuna *inspection* ya kutosha. Binadamu tunapotumia tunaathirika. Tunaomba katika mambo ya *food staff checking* iwe ya haraka, wapitie kwenye hayo maduka na bidhaa zihakikiwe na kama hizi zitaonekana kwamba hazifai kwa matumizi ya binadamu au aliyezileta baada ya kufikishwa katika Mahakama aamriwe azirejeshe alikozitoa kwa sababu hata kufanya *destruction* kwenye chakula bado unaharibu mazingira ya nchi. Ukisema ukakitose baharini unaharibu mazingira yetu, ukisema ukipige moto unaharibu mazingira yetu! Kwa hiyo, chakula mara moja aambiwe akirejeshe alipokichukua na apigwe faini ili iwe fundisho kwa mwingine kutokuleta chakula kibovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *electronics*, kama nilivyokwishasema kwamba yanakuja mambo mapya na Watanzania nao wanataka wawe na televisheni, *DVDs, videos, cameras* na mambo mengi tu. Wenzetu China hasa *South* China katika Jimbo la Gauwnzou utaona kuna viwanda vingi sana ambavyo wafanyabiashara wanapoondoka kwenda kule wananunua zile bidhaa. Sasa na wao kwa kujenga tamaa na kutokupata elimu kwa huko wanakotoka kwa Serikali yao na kutokuelewa wanachokifanya wanaweza wakatengeneza vifaa kama hivyo wakatumia *brand* za majina ambayo ni ya kampuni za nchi nyingine, utakuta televisheni ni ya Kichina, kilichobandikwa ni ile sehemu yake ya kuonekana hii televisheni inatoka China lakini ina *Sony, Hitachi, Sanyo* na vinginevyo.

Ndani kule *inspectors* wa *TBS* wanaweza wakaelewa na watu wengi tu na hata Watanzania wengi wanaelewa kwamba bidhaa hizi zikitoka huko zinafanywa namna hiyo waelimishwe wafanyabiashara waache kutumia *brand* hizi. Watumie yale majina ya

Kichina kwa sababu televisheni ni televisheni tu ikiwa ina jina la *Kanchou*, *Waihini* lakini si inatoka China na inaonyesha kwani lazima uiite *Sony* au *Hitachi*. Mbona wanatumia na zinatumika majumbani? Kitu muhimu ni kuondosha ile *brand* tu uwaambie kwamba wasitumie ile *brand* ya watu, hii ni ya nchi ni ya kampuni unaweza ukashitakiwa na sisi na wao wahusika. Tukishawaelimisha wafanyabiashara na raia wakalielewa hilo, raia haja yake ni televisheni tu *wheather it is from* Pemba au *from* Uganda yeye anataka televisheni aweze kustarehe na watoto wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, waelimishwe wafanyabiashara na hili lingekuwa jema zaidi kwa balozi wetu ambaye yuko Beijing, kuwe na Ubalozi mdogo *Gauwnzou* kuweza kuwatanabaisha wafanyabiashara na kuwapa elimu kwamba bidhaa gani na viwanda gani wanaweza wakachukua biashara na kuleta Tanzania bila ya matatizo kwa Serikali yetu. Tukaanza na huko, siyo kumngojea akaja bandarini tukaliona kontena lake lina televisheni *Sony* kumbe ni *production* ya China, halafu sisi tukazi-*dump* baharini au tukaziponda ponda. Na raia yule ile *capital* anayotumia ni yetu, tumjenge katika mazingira aweze kuendelea kibiashara siyo kumrejesha nyuma wengine wakaogopa, hawa wanasaidia *revenue* kiasi kikubwa sana kwa nchi yetu. Ukienda bandarini kuna makontena mengi tu hata wakati mwingine wanashindwa kuyatoa na ndio maana wakatafuta wafanyabiashara ambao ni maarufu; wafanyabiashara ambao ni wazuri wa biashara ndio wakapewa ruhusa ya kupitisha makontena yao haraka haraka ili *revenue* iingie katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na vitisho tukawarudisha nyuma tukawawekea vikwazo tutazuia *revenue* ambayo inasaidia katika maendeleo yetu ya kila siku na hata wao wanavyouza vifaa katika maduka yao wanatoa *warrant* kwa mwaka mzima, unaenda na televisheni yako miezi mitatu au minne unaporejesha anakupa nyingine.

Unaporejesha anaweza akakupa pesa kwa sababu gani? Anajua ni kifaa kizuri ambacho unaweza ukatumia kilichokosekana kwamba kaitumia *brand* ya watu. Lakini China sio kwamba vitu vyote vibovu, China wanatengeneza vitu vingi, *it is a nuclear power nation,* itakuwa na uwezo wa kutengeneza *nuclear* washindwe kutengeneza televisheni? Ni mambo ya ajabu tu hayo. Tuwajengee mazingira ambayo wao waweze kufanya biashara na kuendeleza mitaji yao ili wakue kibiashara.

Jambo lingine ni vitu vya *electrical*, mimi nasikitika sana kwa sababu vitu vya *electrical,* kuna vitu ambavyo unaweza ukavinunua kutoka nje lakini vikawa na kiwango na kuna vitu unaweza ukavinunua nje lakini visiwe na viwango. Lakini kwa nini tununue vitu vya nje ambavyo havina viwango wakati Tanzania kuna viwanda ambavyo vinatengeneza bidhaa zile za umeme? Nyaya za umeme ambazo ni *weak* kutoka nje, sisi tunatengeneza zilizokuwa nzuri. Ni Shirika la *TANESCO* kuwaelimisha wafanyabiashara ambao wanaleta vifaa vya *electrical* ili waweze kuleta bidhaa ambayo inakubalika katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, unakwenda kununua saa, *engine circuit brake* unaiweka katika nyumba yako, inapotokea *fault* ya umeme inashindwa kurusha

umeme kuondosha umeme katika nyumba, kumbe si *circuit brake* yenye kiwango. Kwa hiyo, sisi tuagize *circuit brake* kutoka katika nchi ambazo zina viwango na vitu kama hivi na mambo kama ya *main switch*, ni bora hata shirika la umeme wakapewa dhamana hii wakati mtu anapo-*apply* kutia umeme katika nyumba yake apate kifaa kilichokuwa na *guarantee;* kilichokuwa na *warrant;* kilichokuwa na uhakika kutoka katika shirika la umeme. Tukaacha vitu vidogo vidogo lakini vitu ambavyo vinaweza vikaleta athari vikapoteza nyumba, vikaleta athari ya moto ikawa ni *cost* kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba sana kwamba nchi yetu tuwe makini na marebisho ya hizi sheria, tusizichukulie kimabavu, tutawaumiza wananchi wetu. Sasa hivi tunapitisha *amendment* hii lakini itatumika baada ya muda gani? Kwa sababu sasa hivi bidhaa ziko madukani, nyingine ziko ndani ya meli zinakuja; nyingine ziko bandarini zinakuja; nyingine ndiyo mtu yuko China ananunua. Sasa hivi nyingine ziko bandarini.

Wapewe muda waelimishwe waambiwe namna gani ya kuhodhi hizi biashara na hata hii ya kusema kwamba kuna huyu *chief inspector* ambaye atatunga kanuni za kuweka taratibu za kukamata na kuhifadhi, tunakamata namna gani, tunakwenda duka moja moja, tunakwenda katika mtaa wa Msimbazi, tutazoa. Ukishauza gari likapakia bidhaa ya Mheshimiwa Mnyaa, bidhaa ya Mheshimiwa Hemed, bidhaa ya Sanya, utakwendaje kuzibagua kule kwenye lile ghala?

Mheshimiwa Naibu Spika, azima tuwe na maghala ya kutosha tuweze ku-*locate areas* kwamba hii ni bidhaa ya mfanyabiashara gani na kuwe na muda wa kuendesha hizi kesi vilevile kwa sababu ile ni *capital* anafanyia biashara, kwa hiyo, na muda wa haraka haraka kuweza kujua biashara ile anaweza akaipata mwenyewe au haipati kwa muda gani.

Nyingine *perishable*, sisi tuangalie biashara za haraka kuweza kuzidhibiti ni biashara za madawa na za chakula, lakini kuhusu *electronics* na *electrical* nafikiri kuwe na muda wa kupata na elimu vilevile wao. Kwa sababu mimi nafikiri kama televisheni yoyote ukaitoa nembo yake ikiwa si *sonny*, au sio ya China au *from* India, from Algeria, ukishaitoa ukafungua ikaonyesha *screen* kwamba anaonekana Mheshimiwa anazungumza kwenye *screen*, hawezi mtu yeyote akakwambia hii ni televisheni ya China au ya Japan kwa sababu *is just a television*.

Mimi ndio nikasema kwamba *recently* nilikuwa Msimbazi yanapita magari yanasomba somba yale ma-*dish, satellite*, yanakwenda kupelekwa kwa nani? Turekebishe sheria zisije zikaleta mwanya mpya wa rushwa kwa sababu zinaweza zikaleta mwanya mwingine wa rushwa tukaanza kuwaadhibu raia wetu wafanyabiashara, tukawarejesha nyuma wakati wao wana nia nzuri baada ya milango ya biashara kufunguliwa.

Hii ni nchi yetu sote, tuingize bidhaa zenye viwango, tusafirishe bidhaa kwa kupata *foreign exchange* lakini vilevile tuwa-*encourage* wafanyabiashara wetu kwamba Serikali ipo pamoja na wao, tuwaelimishe, kwani tukiwaita tukawafahamisha nini lengo la marekebisho ya sheria hii, nani atakataa, lakini wakati ule tutaondoa ile dhiki ya

kwamba na Mtanzania wa kawaida naye anataka televisheni; naye anataka *camera* kwani mtu wa kijijini hataki kupiga picha bwana! Anataka kupiga picha, anataka televisheni amwone Mbunge wake anazungumza nini, anamtetea vipi, anataka kula chakula kizuri. Tuwe na taratibu nzuri za kuhodhi biashara katika nchi lakini kidogo kidogo ili tuweze kufikia lengo tusije tukafanya pupa katika nchi lakini kidogo kidogo ili tuweze kufikia lengo.

Tusije tukafanya pupa tukawazuia wafanyabiashara wakaja wakachuliwa wakapelekwa nchi nyingine za jirani kwa kisingizio cha biashara Afrika Mashariki. Lazima tuwajenge jenge hawa wabaki waendeshe biashara na waweze kuisaidia nchi yetu na kuwa na *revenue* ya uhakika. Mimi naona ni nzuri hii inayoweka kwa sababu ni maslahi yetu na vizazi vyetu lakini vilevile tusichukue gharama kubwa za kuanza kuleta bugudha na kwanyang'anya mali zao vijana wetu ambao tayari wana mwamko mzuri wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia. Nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walioongea kabla yangu kutumia fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwa niaba ya wananchi waishio Kyela kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Waziri Mkuu, kwa Spika na wewe Naibu Spika, vilevile familia, ndugu na jamaa kwa msiba wa Mbunge mwenzetu, Marehemu Salome Mbatia. Mungu aiweke roho yake pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, wasemaji waliotangulia wengi wakiwa wanasheria wamejadili maeneo kwa ufasaha. Ninaona nisije nikarudia rudia basi niongelee sehemu ndogo ya Sheria ya Kanuni za Adhabu , Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 inapendekezwa kufanyiwa marekebisho katika kifungu cha 131. Lengo ni kuondoa kifungu kidogo cha (3) na kuweka kingine kipya. Mimi kwa kifupi sina tatizo kabisa na maudhui ya mabadiliko yanayopendekezwa. Sina tatizo, langu mimi ni matumizi katika sheria yetu ya Kanuni za Adhabu na vilevile mabadiliko tunayoyapendekeza hapa ya neno *rape*, yaani kubaka kwa mtoto mdogo wa miaka kumi na kushuka chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Muswada wenyewe unasema kifungu kidogo kipya kiseme, *subject to sub section two a person who commits an offence of rape of a girl under the age of ten years* na kuendelea, mimi hii inanipa tabu kidogo, kwa sababu naamini ninavyoelewa mimi *rape* au kubaka ni kitendo cha ngono ya kushurutisha, kitendo kilichokosa ridhaa ya mtu wa pili.

Sasa maana yake ni kwamba ikiwepo ridhaa hakuna *rape,* hakuna kubaka na unapoitumia kwa mtoto mdogo wa miaka kumi na kwenda chini unaweka *presumption* kwamba mtoto alikuwa na nafasi ya kutoa, kukataa au kuridhia kitendo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tunajichanganya. Namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuwe *consistent* maana naona sheria zetu zimeanza kutumia maneno mbalimbali na tunafika mahali tunajichanganya. Nitoe mfano mmoja mdogo tu, sheria yetu hiyo ya jinai inatambua kuwa mtoto wa miaka kumi hiyo inayotajwa na kurudi chini hana hata uwezo wa kutenda hata kosa la jinai. Akiokota bunduki pale akakutandika nayo kichwani basi mwenzetu ndiyo mwisho hapo. Lakini huwezi kumpeleka popote kwa sababu sheria yetu inaamini kwamba tendo la jinai linatokea pale tu ambapo vitu viwili vinakuwepo, kitendo chenyewe na dhamira ya kutenda kitendo hicho. Sasa mtoto hana dhamira hiyo ndiyo maana tunamwita *doli incapax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unapozungumzia kwamba *rap* ya mtoto wa miaka kumi tayari unaingiza *presumption* kwamba mtoto angeweza kuridhia au kukataa. Ndio maana nasema tunajichanganya kwa sababu ukiangalia kifungu cha 137 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, kama sijakosea, maana mwenzangu nafikiri atakuwa na *Penal Code*, kinaongelea kitendo cha ngono cha lazima kwa mtu ambaye ana ugonjwa wa akili au kichaa.

Sasa pale hatutumii neno tena *rap*, tunatumia neno *defilement* na mimi nadhani *defilement* ndio *appropriate* kuitumia hapo, na ningemwomba pengine Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kweli aliangalie hili kwa ndani kwa sababu *defilement* maana yake ni kunajisi. Ni kuchafua kitu kilichokisafi kukitia dosari na kwa mtu ambaye hana akili timamu, mtoto mdogo, kichanga wale hawana nafasi kabisa ya kuridhia, wanaingizwa kwenye huo mchezo na ndio maana ukitumia *defilement* hakuna *presumption*..

Hiyo ambayo nilikuwa naiongelea na vilevile uwajibikaji unakuwa wa *strict liability*. Mwanasheria Mkuu anaelewa kwamba hutahitaji kujua kama alikuwa na dhamira, hapo unapewa tu adhabu moja kwa moja. Naelewa tukishafikia Muswada katika *stage* hii Mwanasheria Mkuu anaweza akasema unajua hii tumenakili Uingereza, sijui wapi, ndiyo *trend*.

Sasa mimi naomba haya mambo ya kunakili nakili tuyaache sasa maana huko huko Uingereza siku hizi watu wenye sharubu ndefu tu na ndevu wanadai wawe na haki ya kuitwa *Mrs*. Jamani tukiigaiga sana haya inakuwa *problem*. Kwa hiyo, tulinde sisi wenyewe utamaduni wetu na kuangalia *legal philosophy* yetu ina-*develop* vipi pole pole. Mimi nasisitiza kwamba kwa kweli tusitumie neno *rape* tutumie neno *defilement*.

Nimalizie kwa hoja nzuri tu aliyoisema msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mwanasheria , Fatma Maghimbi. Amesisitiza sana hapa suala la kuhasiwa kwa wabakaji, kalisisitiza mara mbili na kamalizia kusema wanaume hawataipenda adhabu hii.

Lakini Mheshimiwa Maghimbi ameendelea kusema hata wanawake pia wanabaka watoto wadogo, sasa nilitaka tu kumwomba kwa sababu yeye ni Mwanasheria siku

nyingine akichangia namna hiyo basi atueleze njia ya kuhasi hawa wanawake anaowaongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nawashukuru wachangiaji wote, kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kwa mtoa hoja kuweza kutoa ufafanuzi na pengine angetumia muda huu mchana kuangalia hilo neno *rape* au *defilement* kama anaweza kufanya chochote aka-*discuss* na wenzie halafu pia kuingia kwenye Kamati. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6:52 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. VUAI ABDLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia kwa maandishi.

Napenda kuchangia kuhusu Sheria ya Kanuni za Adhabu. Kuhusu sheria hii napendekeza kuwa elimu itolewe kwa makini kwa kila mtu mwanamme na mwanamke kuhusu ubakaji wa watoto wadogo. Sheria hii iwe wazi kwa Serikali, isiwe na pingamizi kwa mtu yeyote kwa swala la rushwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali itoe adhabu kali.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha kikao mchana tulikuwa na wasemaji wawili na sikuwa na msemaji mwingine kutoka kwa Wabunge. Kwa hiyo, kama hali bado ndivyo ilivyo basi ninamwita mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa kuendesha kwa ufanisi majadiliano ya Sheria ya kuzifanyia Marekebisho Sheria Mbalimbali niliyowasilisha leo asubuhi. Napenda vilevile kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu hapa ndani, michango yao imesaidia sana kuboresha Muswada huu na kupanua uelewa wetu na wananchi kwa ujumla wa dhana mbalimbali zilizojadiliwa katika sheria, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda niwataje kwa majina Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu. Waliochangia kwa kusema hapa Bungeni ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Mohamed Sanya na Mheshimiwa Harrison Mwakyembe. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sheria zinazofanyiwa marekebisho siyo nyingi, Waheshimiwa walitoa mchango wa maoni kwa Sheria ya Alama za Biashara na Kanuni za Adhabu, nianze na maoni yanayohusu marekebisho katika Sheria ya Alama za Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani kuhusiana na sheria hii, Sura ya 85. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walio kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao wamechangia kwa ukamilifu sana wakati tulipowasilisha muswada huu kwenye kikao cha Kamati, Dar es Salaam. Hoja zao zote walizozitoa kwenye Kikao zimezingatiwa na zote zilikuwa za msingi na ndio sababu zimeingizwa kwenye S*chedule of Amendments* ambayo tumetawanya kwa Waheshiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Kambi za Upinzani, hoja ya kwanza ilikuwa kwamba wakati mkaguzi mkuu anapofanya ukaguzi wa bidhaa hizo ambazo tunaziita feki basi pawepo watu wengine pale ili kushuhudia huo ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba kukiuka sheria hii ambayo tumeleta hapa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho ni kosa la jinai, hivyo basi sheria zinazotawala taratibu za upekuzi na ukaguzi wa makosa ya jinai ndizo ambazo zitahusika, hivyo, hakuna haja ya kuweka utaratibu mwingine kwenye sheria hii kwa sababu tayari kuna kanuni ambazo zimewekwa kwenye sheria ambazo tunazitumia sasa hivi.

Kwa hiyo, utaratibu wa ukaguzi na upekuzi utafanywa akiwepo mlinzi wa amani wa sehemu husika na watakuwepo watu wengine wale ambao wametajwa kwenye sheria ambazo hivi sasa zimetumika katika ukaguzi wa mali. Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi mtoa hoja kwamba taratibu zote za upekuzi zilizopo kwenye sheria yetu zitazingatiwa wakati wa upekuzi utakaofanywa na huyu C*hief Inspector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa jukumu la mtu anayepatikana na bidhaa feki kutoka chanzo cha bidhaa yaani *supplier* akikamatwa basi analazimishwa kumtaja *manufacturer* alikuwa ni nani. Nilivyosikia hoja ya Msemaji wa Upinzani kama nimeipata vizuri anasema kwamba tunamuonea huyu *supplier* kumwambia kwamba ataje *manufacturer* na kama hatamtaja basi yeye ndiye ataonekana ndiye *manufacturer*. Tunachosema hapa ni kwamba kwanza utengenezaji wa bidhaa hizi feki ni kosa la jinai na mara nyingi hufanywa kwa kificho kwa sababu hiyo siyo rahisi kwa mkosaji kutoa taarifa bila shinikizo. Kwa hiyo, ndiyo sababu tunampa yule ambaye tunamkamata na mali jukumu la kumtaja yule ambaye amenunua mali kutoka kwake yule *manufacturer* na ukweli ni kwamba hata sheria hii inampa siku 14. Anapewa siku 14, kama baada ya siku 14 atashindwa kumtaja yule mtu ambaye ni *manufacturer* wa bidhaa alizokamatwa nazo, ndiyo sheria inasema kwamba tuta-*presume* kwamba yeye ndiye alikuwa *manufacturer*. Hivyo, muda umetolewa ni siku 14, kwa hiyo, siku 14 anatakiwa yule atakayekamatwa na zile mali ajitahidi kumtafuta yule *manufacturer*, siku 14 zikiisha tu hajampata basi sheria ina-*presume* kwamba yeye ndiye alikuwa *manufacturer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kuhusu bidhaa feki, ni kweli kabisa kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu suala hili. Lakini Serikali siyo kwamba imekaa tu hivi hivi, kwanza, ilikwishatoa tangazo kupitia vyombo vya habari mnamo tarehe 14 Julai, 2005 ambalo lilifafanua maana ya bidhaa feki na madhara yake kwa binadamu na uchumi wa nchi.

Pia tangazo hilo lilitolewa na Waziri wa Viwanda na Biashara wakati huo Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa ambalo lilitaja kwamba sheria hii ingeanza kutumika tarehe 14 Oktoba, 2005. Kwa hiyo, ni kusema kwamba wafanyabiashara walipewa *notice* ya miezi mitatu kujitayarisha ili sheria ile ikianza kufanya kazi wasije wakaathirika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Tume ya Ushindani imekuwa ikitoa taarifa mara kwa mara kuhusu bidhaa feki. Tunakumbuka kwamba tarehe 10 - 11 Oktoba, 2007, Tume ya Ushindani ilishirikiana na Shirika la wenye viwanda *(CTI)* na kufanya kongamano katika Hoteli ya *Moven Pick* kwa ajili ya kueleza kwa kina uchambuzi na athari za bidhaa feki katika uchumi wa nchi na kongamano hilo lilitangazwa katika vyombo vya habari, *TV* pamoja na magazeti. Kwa hiyo, nina hakika Taasisi husika pia zimesikia hivyo nadhani zitaendelea kulifanyia kazi suala hili na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kuhitimisha haraka kesi zinazohusu wafanyabiashara ili uchumi usiathirike. Kama mtakavyokumbuka tumempa Waziri kwa sheria hii inayofanya marekebisho, uwezo wa kutengeneza kanuni. Sasa kanuni zitakazotungwa madhumuni yake hasa ni kuweka utaratibu wa kushughulikia masuala yote, yawe ya uwazi na haraka zaidi. Katika kanuni atakazotunga Waziri mambo yote haya yatazingatiwa. Pia tukumbuke kwamba mtu yeyote ambaye ataathirika na uamuzi utakaotolewa na *Chief Inspector*, basi anaweza kupeleka rufaa yake kwenda kwenye Baraza la Ushindani na lile Baraza kwa sababu ndio limeanzishwa, nadhani shughuli zake siyo nyingi sana. Kwa hiyo, nina hakika akipeleka rufaa yake kule atashughulikiwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgongano wa maslahi ya Mkaguzi Mkuu, imetolewa hoja hapa kwamba huyo Mkaguzi Mkuu aangaliwe isije ikawa kwamba tunateua Mkaguzi Mkuu ambaye tayari amekwishakuwa mfanyabiashara. Tunasema hivi, huyu mkaguzi mkuu atahusika na sheria za maadili ya viongozi, atakuwa ni mtu ambaye ni *senior.*

Nina hakika kwamba utaratibu uliopo kwenye sheria ile utahakikisha kwamba tunateua mtu ambaye hatakuwa na *interest* na vile vitu ambavyo atavifanyia kazi na kama atakuwa na *interest* sheria inasema wazi kwamba lazima aeleze na asighulikie kitu ambacho yeye mwenyewe ana *interest* nacho. Na tunaweza kusema kwamba mkaguzi mkuu sasa tunayemfahamu ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani, ambaye tayari sheria yake ya ushindani imebainisha misingi inayotakiwa kufuatwa kuhusu maslahi yanayohusika. Kwa hiyo, jambo hili pia limekwishafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za utunzaji na kuharibu bidhaa, kama nilivyosema ni kwamba kuna kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri mhusika sheria hii inampa uwezo wa kuzitunga, kwa hiyo, katika kanuni hizo pia suala hili litazingatiwa. Hizo zilikuwa ndizo hoja za upande wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja za Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, nadhani yeye kama nimemwelewa vizuri alikuwa anaelezea zaidi kuhusu elimu kwamba ipo haja ya kuwaelimisha ndugu zetu wafanyabiashara kuhusu sheria hii na kuhusu bidhaa feki. Nadhani kama nilivyosema, kazi imekwishaanza kufanyika, tayari wenzetu wa Tume ya Ushindani ya Biashara wanajishughulisha sana kueneza elimu juu ya hizi bidhaa feki.

Kuhusu suala hili la bidhaa feki za chakula na madawa Serikali inatambua athari kubwa zinazoweza kusababishwa na bidhaa hizi. Pamoja na Tume ya Ushindani kushughulikia suala hili pia kuna chombo kingine mahususi ambacho kinasimamia suala hili, nacho ni Mamlaka ya Chakula na Madawa *(TFDA)* inayofanya kazi hiyo hiyo.

Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kupitia Tume ya Ushindani, kuna kikosi cha kazi ambacho kimeundwa ambacho kazi yake kubwa ni kudhibiti bidhaa feki za chakula na madawa. Kikosi hicho maalumu kinahusisha vyombo vingine ambavyo ni *TFDA*, Shirika la Viwango vya Biashara (*TBS)*, Mamlaka ya Mapato *(TRA)*, Polisi na Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, tunawataka wafanyabiasha wote wa chakula na biashara wawe na uzalendo wa kufanya biashara halali ili kunusuru Taifa katika majanga yanayoweza kuzuilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine aliyotoa Mheshimiwa ni kuhusu kuwapa muda na kuwalea wafanyabiashara wa bidhaa feki za *electronics* na vyombo vya umeme. Kama nilivyosema hapo awali Waziri wa Viwanda na Biashara alishatoa *notice* kwa wafanyabiashara kutokujihusha na bidhaa feki tangu mwaka 2005.

Kujihusisha na bidhaa feki ni kosa la jinai na utekelezaji wake hauwezi kuwa wa rejareja, bidhaa feki ni wizi na udanganyifu wa kutumia alama na majina halali ya biashara kwenye bidhaa ambazo hazijatengenezwa na wenye majina hayo. Matumizi ya majina au alama bandia katika bidhaa ni njia ya kukwepa uwajibikaji kwa madhara yanayoweza kutokana na bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utengenezaji wa bidhaa hizo huwa ni kwa gharama ndogo na mazingira hafifu mambo ambayo yanamuathiri mlaji kwa kulipa bei ambayo hailingani na thamani halisi ya bidhaa hizo. Aidha, bidhaa hizo feki za *electronics* za umeme ndio moja ya vyanzo vikuu vya majanga ya moto hapa nchini, kwa sababu hiyo, Taifa lisivumilie bidhaa feki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kila Serikali inapolegeza usimamizi wa sheria hii dhidi ya bidhaa feki, wafanyabiashara wa Kimataifa nina hakika wanaiweka Tanzania katika orodha ya nchi za kupeleka bidhaa feki (ku-*dump)* bidhaa zao hapa kwetu. Nchi yetu haiwezi kukubali jambo kama hilo na

linatakiwa lifanyiwe kazi na ndio maana tumeleta haya marekebisho ya sheria hii, Sura ya 85.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye suala la kisheria kuhusu marekebisho ya Sheria ya Kanuni za Adhabu. Yametolewa maoni mawili katika marekebisho katika sheria hii. Hoja ya kwanza imetolewa na Mheshimiwa Fatma Maghimbi. Yeye ni mwanasheria mwenzangu na msomi, ameuliza je, hili kosa la ubakaji lililotajwa katika kifungu cha 131(3) linahusu wasichana peke yao na haliwahusu wavulana, kwa maana hiyo wavulana hawawezi kubakwa? Yeye anapendekeza litumike neno *child* badala ya *girl*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisheria kosa la kubaka kwa mujibu wa kifungu cha 130 lipo wazi kabisa, ni kosa linalohusu mwanamme kumbaka mwanamke. Kosa lenyewe la ubakaji limeainishwa katika kifungu kidogo cha 130 (2). Vitendo vyote hivi vinaweza tu kufanywa na mwanamme kwa mwanamke, *rape* ni kati ya mwanamme na mwanamke siyo kati ya mwanamme na mwanamme.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa msomi mwenzangu kwamba eneo hili halijaachwa wazi, kipo kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu ambacho kinakataza vitendo vilivyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge. Pale ambapo vitendo hivyo vinafanywa kinyume cha maumbile mhusika anawajibishwa kijinai na adhabu yake ni kifungo cha maisha. Pale ambapo vitendo hivyo vitafanywa kwa mtoto mdogo mhusika atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka 30 na mtu atakayejaribu kufanya vitendo hivyo pia kuna adhabu imewekwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, ambayo ni kifungo kisichopungua miaka 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu hizi zimewekwa kwa mujibu wa sheria ya *SOSPA* ya mwaka 1998 ambayo ndiyo tunairekebisha. Kutokana na maelezo hayo, bila shaka eneo hili pia tayari lina adhabu kali isipokuwa hapa sio mahali pake.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili limezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, mwanasheria mwenzangu tena msomi mzuri kabisa. Yeye amehoji kosa la kubaka, *rape* kwa mtoto wa umri wa miaka 10 badala ya kosa tulilolizoea la *defilement*. Bila shaka Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba sheria hizi chimbuko lake ni huko Uingereza au kama alivyosema yeye mwenyewe, kosa la *defilement* linaonekana kuwa ni dogo ukilinganisha na kubaka na vilevile utaratibu wake wa kuliadhibisha ni mgumu zaidi na baada ya tafiti nyingi kufanyika ilionekana kwamba msingi wa makosa haya ya *statutory rape* ni kukosekana kwa ridhaa ya dhati. Mtoto mdogo mwenye umri huo kwa vyovyote hawezi kutoa ridhaa iliyokuwa thabiti na kwa sababu hiyo hapaswi kuguswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la kuwalinda watoto hatuna huruma, tutaendelea kuwa wakali, lakini vilevile ninamshukuru Mheshimiwa mwenzangu, Dr. Mwakyembe kwa kunikumbusha kwamba kosa la *defilement* bado lipo kwa wanawake wasiokuwa na akili timamu katika kifungu cha 137 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu. Hata hivyo, naomba nimkumbushe kwamba kwa upande huo yametumika maneno

yaliyotumika katika fungu hilo yanayojumuisha maneno yafuatayo, *not amounting to rape*. Kwa hiyo, kosa la *defilement* limebakizwa tu kwa watu wa namna hii kwa vile vitendo ambavyo siyo *rape* vinginevyo hata kwa watoto wadogo wa namna hii watalindwa na sheria ya *rape.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Maghimbi kwamba watu wanaopatikana na hatia ya kosa la kubaka wapewe adhabu ya kuhasiwa, utekelezaji wa hoja hii una ugumu. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mheshimiwa Maghimbi wanakumbuka kwamba hoja hii ilikuwepo wakati wa kutunga sheria hii lakini haikuweza kutekelezwa kutokana na masharti ya Ibara ya Katiba, Ibara ya 13(6)(e) ianyokataza adhabu za kutweza. Bila shaka adhabu ya kuhasi ni mojawapo ya adhabu zinazokatazwa chini ya Ibara hii ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**Waziri wa Maji:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2007
***(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 2) Bill, 2007)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara ya 7

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nisingependa kuingia kwenye malumbano ya kisheria hapo lakini nilikuwa ninamwomba tu pengine *Attorney General* baadaye akae na wataalamu wake waiangalie tena hii Ibara ya 10. Nadhani wala hakunielewa nilikuwa nataka kusema nini, pengine nirudie tena lakini kama hataelewa siyo vibaya tukaipitisha lakini baadaye akae tu na wanasheria waingalie upya.

Nilichokuwa ninakisema ni kwamba unapotumia *offence* ya *rape* kwa mtoto mdogo, mtoto wa miezi miwili au mitatu mpaka miaka kumi, *rape* ina-*import presumption* ya kwamba yule *victim* alikuwa na uwezo wa kukataa, ndio maana nilisema toka mwanzoni kwamba tumefika umri sasa hivi Watanzania tumekomaa katika kila taaluma hatuhitaji kuendelea kuchukua mifano ya Uingereza mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa, hili kosa lazima lionekane tofauti na kosa la mtu mzima. Mtoto mdogo wa miezi mitatu kosa lake lile akitendewa ni kosa ambalo halihitaji hata *argument* katika Mahakama kwamba je, aliridhia vipi, hilo ni *strict liability* na nimeeleza kama halijaeleweka basi tutaendelea kujadiliana huko mbele. Mimi nasikitika tu kwamba halijaeleweka lakini ni suala ambalo mimi mwenyewe nimefundisha *criminal law* kwa zaidi ya miaka 15, wanafunzi wangu wote wanaelewa hilo suala ninalolisema. Ahsante sana! (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nimemwelewa sana Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na sisi wenyewe ni wasomi, lakini hata hivyo namhakikishia kwamba tutaliangalia tuwasiliane ili tuweze kuona namna ya kuboresha hicho kitu anachokizungumzia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hapana! Tunatunga sheria jamani, tunaboresha wapi? Tunaboresha hapa, tunaboresha kwenye Muswada! Hamuwezi kusema mtaboresha nje ya hapa na inaruhusiwa na wengine kujadili pia hili, tunatunga Muswada ukisema tunaboresha tunaboresha wapi sasa? (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi msimamo wetu wa Kiserikali ni huu ambao nimeuzungumzia wakati nilipokuwa najibu

hoja ya Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kwa hiyo, bado tunasema kwamba hii ni *statutory rape* tofauti na *defilement*.

**MWENYEKITI:** Tofauti zake nini? Tusaidie!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba *concept* anayozungumzia mara nyingi inahusika kwenye utendaji wa kosa, hapa tunazungumzia juu ya kutendewa kitendo cha jinai. Huyu mtoto mdogo ni *victim* na yale mambo anayotenda yule mkosaji sasa ili kulipa hili kosa umuhimu unaostahili ndio sasa tumetumia neno *rape* badala ya *defilement.* Kwa hiyo, ni uamuzi wa Serikali kutumia neno hilo *rape* badala ya kutumia neno *defilement*.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani wanasheria wasitukanganye, tuandikiwe yale maneno yanayochukua maana ya tatizo. Kama *defilement* inaonesha wazi huyu hakuwa na uwezo hata wa kusema lazima iwe *defilement*, kama *rape* inaonyesha kwamba huyu angeweza kukataa, ibaki *rape* kwa sababu huyu mtoto tukianza kufanya *rape* watu wataweza kutoroka kwa kusema mtoto yule si angepiga kelele!

Kama kunaleta utata wowote wanasheria hapa hapa mlimalize, tusizunguze mambo ambayo ni mabaya, ni *serious* na ile *concept* ya kusema *defilement* maana yake ni *victim* hata anayekuwa *raped is a victim, a very serios victim*. *Rape in marriage, rape everywhere* ni dhambi kubwa lakini kwa huyu mtoto tunachokitafuta kusiwe na utata kafanyiwa mambo ya ovyo, *straight* huyu mtu apelekwe tena nashangaa haikuwekewa kifungo cha maisha, huyu anapaswa kufungwa maisha *immediately*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilivyozungumza ni kwamba *defilement* ni kosa dogo kuliko *rape* au zaidi ya hapo. Ukweli ni kwamba yule mtoto mdogo mtu yeyote atakayemwingia ni *rape,* haihitaji kusema kwamba mtoto alikubali au hajakubali, akimwingia tu ni *rape* na hilo tumefanya makusudi ili kufanya kosa hili liwe kubwa ili adhabu inayopendekezwa ioane na kosa lenyewe.

Zaidi ya hapo ni kwamba uthibitishaji wa kosa la *defilement* ni mgumu zaidi kuliko kosa la *rape,* kosa la *rape* ni kuingia tu, *defilement* inatakiwa mpaka ufanye vitu vingine zaidi ya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo sababu Serikali imeona kwamba ni vizuri kosa hilo liendelee kuitwa kosa la *rape* na siyo *defilement*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii ni kanuni. Kama Mheshimiwa Dr. Harrion Mwakyembe angekuwa ameamua kwamba anaomba kutoa hoja, angeleta *schedule of amendments* na tungepiga kura. Lakini kwa sababu ametaka ufafanuzi tu, ndio maana tumeruhusu wazungumze lakini bado *owner* anabakia Serikali kwa kwa sababu hakukuwepo na *schudule of amendmets* ambayo ingekuwa ni hoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe hakutoa hoja alitaka ufafanuzi, angetoa hoja tungepiga kura, kama Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe angeshinda basi Serikali ingebidi ikubali yale tuliyofanya sisi lakini kwa sababu alitaka ufafanuzi tu nimeruhusu majadiliano lakini bado *ownership* iko kwa Serikali kwa sababu hakukuwepo na hoja. Nadhani tumeelewana.

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2007 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali *(Na.2)* wa mwaka 2007 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2007)* na imeukubali pamoja na mabadiliko yake. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na *Order Paper* yetu ya leo Shughuli za Bunge zimekwisha. Ningependa kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Nyaulawa alipokuwa katika mkutano wetu wa *SADC* alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *SADC* inayohusika na mambo ya *HIV/AIDS. (Makofi)*

Kwa hiyo, tunafurahi kwamba katika eneo la *SADC* Tanzania ni Mwenyekiti, katika *network* ya UKIMWI kwa Wabunge katika Bara la Afrika Tanzania ni Mwenyekiti. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na *TAPAC* yenyewe ni mfano katika Mabunge mengine yote Duniani. Kwa hiyo, tunadhani Waheshimiwa Wabunge mtachukua nafasi hiyo kila watu kwenye *constituency* zao kuitumia *TAPAC* yetu na *good will* ya watu wengi kutusaidia katika suala hili UKIMWI.

Nadhani Wabunge wa Majimbo na Wabunge wa Viti Maalumu washughulike na hizi *network* kusudi kuweza kujenga rekodi inayokubalika kwa sababu hawezi kuongoza Bara, tukaongoza na *SADC* halafu tusionekane mfano kabisa. Kwa hiyo, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote tujirikishe na *TAPAC* yetu. Kuna mipango mingi sana itakayotusaidia kama Wabunge ndani ya Majimbo yetu kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha kikao mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 11.36 Jumanne, Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano Tarehe 31 Oktoba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*